SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa


UKURASA 3




## Bashungwa aagiza Kigogo wa TARURA kuvuliwa madaraka

# MAISHA

JANUARI 23, 2022
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14
FURAHIA LADHA
Juice ya Karoti, Tangawizi, Nanasi



Ukurasa 14
UREMBO:
VIKUKU
Pambo la kale linalodumazwa



KATUNI
Ukurasa 16



Mambo ya kuzingatia kabla ya kuuza nyumba
Ukurasa 15


# Nipashe

Jumapili Januari 23, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • No. 0580834
www.ippmedia.com
JUMAPILI
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Mafuvu ya machifu kurejeshwa nchini

**Rais** asema mchakato umeanza, mabalozi na watu mashuhuri kutangaza utamaduni wa Tanzania...*Endelea ukurasa 2*



Chifu Mkuu wa Kabila la Kichaga, Frank Marealle, akikabidhi ngao na mshale kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kama ishara ya kumkaribisha rasmi kwenye kabila hilo, wakati wa uzinduzi wa tamasha la kwanza la Utamaduni wa Mkoa wa Kilimanjaro, katika Uwanja wa Chuo cha Ushirika Moshi, jana. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 4

### UJENZI MAGOMENI KOTA ASILIMIA 100

SERIKALI imetangaza kukamilika kwa mradi wa nyumba za Magomeni Kota na kuahidi siku yoyote kuanzia sasa, wananchi...

UKURASA WA 4

### WAKULIMA MAPARACHICHI WAPATA SOKO INDIA

SHIRIKA la Ndege la Tanzania (ATCL), limeanza kusafirisha maparachichi kwenda India huku tani mbili zikiwa zilisafirishwa juzi...

UKURASA WA 4

### WAZIRI ATAKA UTATUZI KERO UPATIKANAJI DAWA

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameiagiza Bohari Kuu ya Dawa (MSD), kutatua kero ya upatikanaji wa...

## Watu 16 mbaroni madai kufukua, na kuiba mwili wa mtoto mdogo

UKURASA 2

## Mwalimu mstaafu auawa, mwili wake watupwa pembeni mwa barabara

UKURASA 3

MICHEZO TANZANITE KUIVAA ETHIOPIA UK.23
MAONI, KATUNI UK.6

## Mifugo 1,200 yafa kutokana na ukame

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kagaigai, amesema ukame ambao umeendelea kuwa tishio nchini, umesababisha vifo vya zaidi ya mifugo 1,200 katika mkoa huo.

Alikuwa akitoa taarifa ya hali ya mkoa huo jana kwa Rais Samia Suluhu Hassan, aliyekwenda mkoani hapo kuzindua Tamasha la Utamaduni wa Kilimanjaro.

"Mheshimiwa Rais, Mkoa wa Kilimanjaro unakabiliwa na ukame, hasa katika maeneo ya Mwanga na Same. Hali hiyo imesababishwa na kukosekana kwa mvua na hali hiyo imesababisha kufa kwa ng'ombe 841, kondoo 406 na punda 10," alisema

Wiki iliyopita, serikali ilitangaza maafa kama hayo ya kufa mifugo 62,593 katika wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, kutokana na kukosa maji na malisho, baada ya ukame kuvikumba vijiji mbalimbali katika wilaya hiyo.

Kutokana na taarifa hiyo, Rais Samia alielezea masikitiko yake kuhusu hali ya ukame na vifo vya mifugo.

"Wakati tumekusanyika kufurahia tamasha hili la Mkoa wa Kilimanjaro, tamasha hili limetokea wakati nchi yetu imekumbwa na maafa yatokanayo na ukame, hususani katika maeneo ya wafugaji na wakulima.

"Nina taarifa kwamba Oktoba, mwaka jana, wakulima walishindwa kupanda mazao kutokana na ukame uliokuwepo, ambao umetokana na kuchelewa kwa mvua za vuli na maelfu ya mifugo imepotea.

"Kwa mkoa huu, natambua wilaya za Same na Mwanga ndio zimekumbwa, hili ni janga kubwa na nitumie nafasi hii kuwapa pole wana Kilimanjaro na mikoa mingine ikiwemo Arusha na Manyara ambako adhari zimeonekana kuwa kubwa zaidi," alisema.

Aliwataka wafugaji kushirikiana na serikali kuona namna bora ya kuanza kufuga kisasa kwa kupanda malisho.

Rais alisema serikali imejiandaa vyema na jinsi ya kupanda malisho bila kutegemea mvua lengo ni kuepuka adhari zinazotokea kwa kusubiria mvua.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk.Hussein Ali Mwinyi (wa nne kulia), akiitikia dua ya kumuombea aliyewahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji ZIPA, marehemu Salum Khamis Nassor, wakati ikisomwa na Mufti Mkuu wa Zanzibar Sheikh, Saleh Omar Kabi, baada ya kumalizika kwa sala ya jeneza, katika Masjid Jamiu Zinjibar Mazizini jana. Kushoto kwa Rais ni Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein na Makamu wa Pili wa Rais mstaafu Balozi Seif Ali Iddi na (kulia kwa Rais) ni Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla. **PICHA: IKULU**

# Mafuvu ya machifu kurejeshwa nchini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema serikali inaendelea na majadiliano ya urejeshwaji wa mafuvu ya viongozi wa kimila yaliyoko nje ya nchi, ambayo yalichukuliwa na wakoloni.

Kadhalika, ameagiza mabalozi wanaowakilisha mataifa mbalimbali nchini pamoja na watu mashuhuri, kushirikishwa kwenye matamasha ya utamaduni yanayolenga kutangaza asili ya utamaduni wa Tanzania.

Samia alisema hayo jana alipokuwa akizindua Tamasha la Utamaduni wa Kilimanjaro, lililofanyika mjini Moshi.

"Jambo lingine mliloliomba la kurudisha mafuvu ya machifu yalichochukuliwa wakati wa ukoloni ili yaweze kutumika kwenye vivutio vya utalii.

"Tayari tumeanza mazungumzo na Wizara ya Mambo ya Nje ya Nchi na Ushirikiano wa Kimataifa pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii, wanaendelea na majadiliano kuona namna ya kuyarudisha nchini ili yatumike kama kivutio cha utalii na tukishafanikiwa tutawajulisha," alisema.

Kuhusu utamaduni, alisema ni ajira na utalii na kwamba nchi itapata heshima zaidi kutokana na utamaduni wake ndani na nje ya nchi na kuvuta watu mbalimbali kuja kuuona, hivyo kukuza pato la taifa.

"Uzoefu huko duniani unaonyesha kuwa matamasha kama haya, yakiandaliwa vyema yanaweza kuvutia watu wengi zaidi duniani kufika kila mwaka kuona utamaduni wetu. Ziko nchi nyingi zaidi zenye matamasha kama haya ikiwemo Brazil.

Kuna tamasha linalovuta watu wengi pia huko Ujerumani. Huvutia zaidi ya watu milioni tano hadi sita kwa wiki ile ya tamasha.

"Hata kwetu tuna Tamasha la Zanzibar, Bagamoyo na hata hili likiandaliwa vyema litavutia watu wengi zaidi," alisema.

Kutokana na umuhimu wa utamaduni, Rais Samia aliwataka viongozi wa mila kuwarithisha utamaduni wa mila na desturi watoto ili kuwasaidia vijana kuiga na kutekeleza kwa faida ya Tanzania yenye zaidi ya makabila 120.

Akijibu risala ya Mangi Mkuu wa Wachaga ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Machifu Tanzania, Frank Marreale, Rais Samia alisema: "Mliomba kuweka taarifa kamili za machifu na mpango wao wa ushiriki wakati wa enzi za ukoloni, mbali na taarifa zilizopo sasa. Idara ya Maendeleo na Utamaduni inaleta programu maalumu ya kuhifadhi taarifa za machifu.

**MAPANGO YA MACHIFU**

Kuhusu utambuzi wa mapango ya machifu, Rais Samia alisema: "Serikali imeshaanza utaratibu wa kuyatambua kupitia machifu na wazee wa kimila ili yaweze kutumika kwenye utalii.

Na mpaka Januari mwaka huu, maeneo 36 tayari yametambulika kama vivutio vya utalii.

"'Nafahamu, wizara tayari imekutana na machifu pale Dodoma na walikubaliana kila mmoja aendelee na utambuzi wa maeneo hayo kwa kutambua maeneo yaliyopo kwenye himaya zao."

Rais Samia alisema kwa kuzithamini mila la desturi njema serikali imeunda wizara mahususi itakayoshughulikia na kusimamia moja kwa moja shughuli za sanaa,utamaduni na michezo.

Awali, Mwenyekiti wa Umoja wa Machifu Kilimanjaro (UMK), Chifu Frank Marriale aliomba serikali kuimarisha na kuhifadhi majengo na vifaa vya zamani vya mila na desturi ili visipotee.

Alisema vinapaswa kuendelea kutumika katika kufundisha, kushauri, kuelekeza, kuhamasisha utamaduni, mila na desturi.

Katika siku za hivi karibuni, alisema kumegundulika nyumba kwenye handaki inayosadikiwa ilikuwa ya Wajerumani maeneo ya Kibosho, na kwamba ni kumbukumbu muhimu inayotakiwa kutunzwa.

Pia alisema liko pango linasemekana limetoka Kibosho kwa Mangi Sina, kupita Old Moshi kwa Mangi Meli na kuelekea Marangu kwa Mangi Marrealle lenye urefu wa kilomita 40, ambalo lilitumiwa kusafirisha watu na wanyama wakati wa vita.

# Watu 16 mbaroni madai kufukua, na kuiba mwili wa mtoto mdogo

**Na Thobias Mwanakatwe**

WATU 16 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Singida kwa mahojiano kutokana na kufukuliwa na kuibwa kwa mwili wa mtoto, Christian Samson, mwenye umri wa mwaka mmoja na mwezi mmoja.

Inadaiwa kuwa mwili wa mtoto huyo ulifukuliwa kwa kile kilichoelezwa ni kutokana na imani za kishirikina.

Mtoto huyo alikuwa amezikwa kwenye makaburi ya Kipondoda yaliyoko kitongoji cha Kipindoda, tarafa na wilaya ya Manyoni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP) Stella Mutabihirwa, katika taarifa yake jana kwa vyombo vya habari, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, jeshi hilo kupitia makachero wake lilifika katika eneo la tukio na kufanya uchunguzi wa awali na kujiridhisha kuwa ni kweli kaburi lilifukuliwa na mwili huo kuibwa huku jeneza likiachwa tupu.

Kamanda Mutabihirwa alisema Januari 18, mwaka huu, saa 1:15 asubuhi, Jeshi la Polisi lilipokea taarifa kuwa usiku wa kuamkia tarehe na mwezi huo, kwenye eneo la makaburi hayo, mwili wa marehemu, aliyekuwa mkazi wa Kipondoda ambaye alifariki Januari 15, mwaka huu, kwa maradhi na kuzikwa siku iliyofuata, ulifukuliwa na kuchukuliwa kutoka kwenye jeneza na watu wasiojulikana. Alisema watu hao baada ya kufanya uhalifu huo, walitokomea kusikojulikana hadi Jeshi la Polisi lilipopata taarifa na kutuma timu ya makachero ambao kwa kushirikiana na viongozi wa kijiji na raia wema, walifanya msako mkali.

Mutahibirwa alisema siku sita baada ya maziko, yaani Januari 21 majira ya saa 6:15 usiku, mwili wa marehemu ulipatikana ukielea kwenye kisima cha maji chenye urefu wa futi 12 kilichoko jirani na eneo la kata hiyo.

"Jeshi la Polisi linawashikilia watuhumiwa 16 kwa mahojiano. Mwili wa marehemu umefanyiwa uchunguzi wa kitabibu katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni na kukabidhiwa kwa ndugu kwa hatua za mazishi," alisema Mutabihirwa.

Kamanda huyo aliwasihi wananchi kuachana na kujihusisha na imani za kishirikina na kutenda matendo mema yanayompendeza Mwenyezi Mungu kutokana na tukio kujionyesha dhahiri kuwa na viashiria vya moja kwa moja vya imani hizo.

# Mwalimu mstaafu auawa, atupwa kando barabarani

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

MWALIMU mstaafu Kassim Shiraz (67), amekutwa akiwa ameuwawa na watu wasiojulikana na mwili wake kutupwa pembezoni mwa barabara ya Songea- Mbinga.

Kutokana na mauaji hayo, Jeshi la Polisi mkoani Ruvuma linamsaka mtu mmoja aliyetajwa kwa jina la Kamongo, fundi seremala, mkazi wa mtaa wa Namanditi katika Manispaa ya Songea.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Ruvuma, Pilli Mande, alisema tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 12:00 asubuhi katika mtaa wa Namanditi kwenye stendi ya mabasi iliyoko kata ya Ruhuwiko.

Kamanda Mande alisema siku hiyo ya tukio kwenye kituo cha mabasi cha Namanditi, Shiraz ambaye alistaafu kazi mwaka 2018, alikutwa akiwa ameuawa pembezoni mwa barabara akiwa amechomwa na kitu chenye ncha kali maeneo ya mgongoni.

Alisema chanzo cha mauwaji ni wivu wa mapenzi kwa madai kwamba Mwalimu Shiraz tangu mwaka 2017 alikuwa na uhusiano na mwanamke mmoja (jina linahifadhiwa) ambaye fundi seremala huyo alianza kumfuatilia na kumtaka uhusiano wa kimapenzi lakini akamkataa kwa madai kuwa ana mpenzi wake ambaye ni Shiraz.

Kamanda Mande alisema fundi Kamongo alimtishia kwa maneno mwalimu huyo mstaafu kuwa atamuuwa jambo ambalo lilimlazimu kutoa taarifa ya kutishiwa kwa maneno katika kituo kidogo cha polisi cha Madizini kata ya Lizaboni.

Alisema mazingira yanaonyesha kuwa mwanamke huyo hivi karibuni alianza kuwa na uhusiano wa kimapenzi na fundi Kamongo na kwamba juzi usiku, majira kati ya saa 3:00 na saa 4:00 usiku, walikuwa kwenye baa moja wote watatu wakipata vinywaji na Mwalimu Shiraz alitoka na huyo mwanamke huku fundi akiondoka peke yake.

Kamanda alisema pamoja na watu hao kuondoka kwa njia tofauti, siku ya pili Shiraz alikutwa akiwa ameuawa na kutupwa kando ya barabara na mwili wake ukiwa umechomwa na kitu chenye ncha kali.

**AHOJIWA TUHUMA MAUAJI**

Katika hatua nyingine, Polisi mkoani Ruvuma wanamshikilia mwendesha pikipiki (jina linahifadhiwa) kwa mahojiano kutokana na mauaji ya kikatili ya Gema Haule (23), mkazi wa mtaa wa Kimoro Makambi, Manispaa ya Songea, aliyekuwa mhudumu wa nyumba ya kulala wageni ya Peace Lodge iliyoko Matarawe.

Kamanda Mande alisema jana kuwa kufuatia tukio lililotokea juzi la mauwaji ya kikatili tayari polisi ilishaanza kufanya jitihada za kuhakikisha kuwa mtuhumiwa wa mauwaji hayo anakamatwa.

Alisema upelelezi wa awali wa polisi umebaini kuwa mtuhumiwa huyo baada ya kumuuwa kikatili Gema kwa kumkaba shingo kisha kumfunga shingoni na kamba za viatu na hivyo kumsababishia kifo, alichukuwa ufunguo wa chumba ambako alifanyia kitendo hicho cha kinyama na kukifunga.

Kamanda Mande alisema upelelezi umebaini kuwa baada ya kuua, mtuhumiwa alichukua nguo, simu zilizokuwa zimechukuliwa na mhudumu baada kushindwa kulipa deni la pango la Sh. 50 kisha alichukuwa kitabu cha wageni na kuchana ukurasa ambao una taarifa zake likiwamo jina kamili la mtuhumiwa.

Alisema mtuhumiwa huyo aliondoka eneo la tukio kwa usafiri wa bodaboda akiwa na ufunguo wa chumba namba 4 ambacho alikuwa amemfungia mhudumu wa nyumba hiyo na kutokomea hadi eneo la kituo cha daladala cha Majengo wakati simu moja aliiacha kwa mmiliki wa gesti hiyo. Mande alisema mtuhumiwa huyo akiwa eneo la Majengo, alimwomba mwendesha bodaboda amsaidie kurudisha ufunguo wa chumba ambao alidai kuwa aliondoka nao kwa kutokujua na mwendesha bodaboda alikubali na kuuchukua ufunguo na kwenda nao hadi kwenye nyumba hiyo ambako alipofika, alikuta umati mkubwa wa watu wakiwamo askari polisi waliokuwa wamefika baada ya kusikia tukio hilo.

Alisema dereva huyo alikabidhi ufunguo akidai kuwa amekabidhiwa na mteja wake aliyedai kuwa amesahau kuurudisha kisha polisi walimkamata kwa lengo la kusaidia upelelezi.

Kamanda alisema baada ya mahojiano, polisi wamejiridhisha na kumwachia kwa kuwa alikuwa hafahamu chochote kuhusiana na tukio hilo licha ya kuwa alimbeba mteja wake ambaye aliomba ampeleke majengo na baadaye kuomba amsaidie kurudisha ufunguo jambo ambalo limeonyesha kuwa hakukuwa na sababu ya kuendelea kumshikilia.

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**LIBERATHA MBASHA MOSSES** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 571 DYE – IST.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MAG/RB/29916/2022.**

# Bashungwa aagiza kigogo wa TARURA avuliwe madaraka

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amemwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, kumrudisha makao makuu na kumpangia kazi nyingine aliyekuwa Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Ibrahim Kibasa.

Meneja huyo alishindwa kusimamia miradi ya ujenzi wa barabara mkoani Ruvuma mwaka 2020.

Bashungwa alitoa maelekezo hayo jana wakati akikagua ujenzi wa Daraja la Ruhuji lenye urefu wa mita 22 na upana wa mita nane lililoko katika barabara ya Mabatini – Ramadhani.

Daraja hilo linaunganisha Kata za Njombe Mji na Ramadhani katika Halmashauri ya Njombe Mji, mkoani Njombe.

Waziri Bashungwa alisema hajaridhishwa na kasi ya ujenzi wa daraja hilo ambalo lilianza kujengwa Mei 21, 2020 na lilitakiwa kukamilika Septemba, 2020.

"Kuna uzembe mkubwa katika ujenzi wa daraja hili ambalo ni kiungo muhimu kwa wananchi wa maeneo haya kwa kuwa wanatumia daraja hili kwa ajili ya kusafirisha mazao yao sokoni, hivyo kususua kwa ujenzi wa daraja hatuwatendei haki wananchi" alisema Bashungwa.

Bashungwa alimwagiza Meneja TARURA Mkoa wa Njombe, Mhandisi Gerald Matindi, kumsimamia mkandarasi anayejenga daraja hilo na kuhakikisha anakamilisha kwa wakati.

Waziri Bashungwa pia alitoa muda wa miezi sita kwa Meneja wa TARURA Mkoa wa Njombe kutatua matatizo ya miundombinu katika mkoa huo.

Akiwa katika Kijiji cha Mbalache wilayani Makete, Bashungwa aliagiza kuanza haraka kwa ujenzi wa Barabara ya Lupila – Kipengere yenye urefu wa kilometa tano kwa kiwango cha changarawe na kutoa wiki mbili mkandarasi kuanza ujenzi huo.

Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Mhandisi Marwa Rubirya, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiongezea TARURA bajeti kutoka Sh. bilioni 8.4 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 22.5 mwaka 2021/22.

A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company

KILIMANJARO
DRINKING WATER

**TAARIFA KWA UMMA**

**BONITE BOTTLERS LTD** inapenda kuufahamisha umma juu ya kusitisha matumizi ya **plastiki laini (seal)** katika vifuniko vya chupa za **Maji ya Kilimanjaro** kutokana na agizo la serikali juu ya matumizi ya plastiki hizi kulinda mazingira.




@kilimanjaro_drinking_water kilimanjarodrinkingwater kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422

## Waziri ataka utatuzi kero upatikanaji dawa

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Afya, Ummy Mwalimu, ameiagiza Bohari Kuu ya Dawa (MSD), kutatua kero ya upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini, kutoka asilimia 50 ya sasa hadi kufikia asilimia 90, ndani ya miezi mitatu.

Waziri Ummy alitoa agizo hilo jana mkoani Dar es Salaam, alipotembelea MSD na kuzungumza na menejimenti kuhusu changamoto za upatikanaji wa dawa nchini.

Alisema amepata changamoto hizo kutoka kwa baadhi ya vituo vya afya na wananchi aliokutana nao na kwamba lazima itatuliwe haraka iwezekanavyo, huku akisisitiza upatikanaji wa dawa muhimu ambazo wananchi wanaandikiwa na daktari.

"Hakikisheni upatikanaji wa dawa muhimu zote katika vituo vya kutolea huduma za afya. Rais Samia Suluhu Hassan alituwezesha kupata fedha za kununua dawa, hivyo hakuna sababu ya ukosefu wa dawa na hili nitalisimamia kikamilifu kuhakikisha dawa zinanunuliwa na kusambazwa kwenye vituo kwa wakati," alisema Waziri Ummy.

Pia waziri huyo ametembelea maghala ya kuhifadhia dawa ya MSD, sambamba na kujionea vifaa mbalimbali vya maabara pamoja na vitendanishi vyake.

Katika hatua nyingine, Ummy alimpongeza Mkurugenzi Mkuu wa MSD na timu yake kwa kufanya vizuri katika kusimamia uanzishaji wa viwanda vya ndani vya dawa.

Aliwataka kuendelea kubuni zaidi aina ya viwanda vitakavyozalisha bidhaa muhimu za afya ili kutatua changamoto za dawa na vifaa tiba nchini.

Pia alielezea kufurahishwa na juhudi za MSD za kuwezesha upatikanaji wa mashine za kusafisha damu kwa bei nafuu ambazo zitapunguza gharama kwa zaidi ya asilimia 50.

# Ujenzi Magomeni kota asilimia 100

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imetangaza kukamilika kwa mradi wa nyumba za Magomeni Kota na kuahidi siku yoyote kuanzia sasa, wananchi waliokuwa wakiishi hapo, watarejea katika nyumba hizo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Aisha Amour, alitangaza kukamilika kwa mradi huo jana Dar es Salaam, alipofanya ziara ya ukaguzi iliyolenga kuangalia mwendelezo wa ujenzi.

Akiwa katika nyumba hizo, Amour alisema kwa sasa mradi huo umekamilika na kilichobaki ni siku yoyote wakazi waliokuwa wakiishi eneo hilo kukabidhiwa funguo.

"Wakati wowote kuanzia sasa wakazi waliokuwa wakiishi hapa wanaweza kuruhusiwa kuingia katika nyumba hizi, kilichobaki kwa sasa ni marekebisho madogo ambayo hayatachukua muda mrefu, lakini kwa sasa mradi umeshafika asilimia mia," alisema Amour.

Katika hatua nyingine, Amour aliwataka wakazi ambao wataingia katika nyumba hizo kuwa watulivu na kuzingatia utunzaji wa miundombinu kwenye nyumba hizo ili kuiepusha serikali kupata hasara za mara kwa mara za kufanya marekebisho.

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), Abasi Kondoro, alimshukuru Katibu Mkuu Amour kutembelea mradi huo na kubainisha mambo kadhaa ambayo TBA imebuni na kuyaongeza.

"Mara ya mwisho tulipokaa katika kikao na wadau katika eneo hili ilikuwa limebakia suala la 'lift' lakini leo tumemuonyesha Katibu Mkuu lift zote 10 katika maghorofa yote, sambamba na hilo pia tumeongeza eneo la uwekezaji machinga complex kwa ajili ya kuwahudumia wakazi watakao kuwa wakiishi kwenye kota hizi.

"Ujenzi huu umetumia fedha za ndani na hii yote ni kwa ajili ya kutengeneza chanzo cha mapato kwa TBA na utekelezaji wa mradi huu umezingatia viwango bora," alisema.

Mwenyekiti wa nyumba za Magomeni Kota, George Abel, aliishukuru serikali kwa kutembelea mradi huo na kuwatoa hofu wananchi, huku akiiomba serikali iwape mikataba ya kuishi katika nyumba hizo ili waanze kuisoma na kuipitia mapema.




Mkaguzi wa Polisi kutoka Dawati la Jinsia na Watoto, Mkoa wa Kinondoni Dar es Salaam, Christopher Newton, akizungumza kwenye mkutano wa kuwajengea uwezo wadau wa kampeni ya 'Safari Salama Bila Rushwa ya Ngono Inawezekana', inayoendeshwa na Shirika la Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wakulima maparachichi wapata soko India

**Na Gwamaka Alipipi**

SHIRIKA la Ndege la Tanzania (ATCL), limeanza kusafirisha maparachichi kwenda India huku tani mbili zikiwa zilisafirishwa juzi.

Akizungumza wakati wa usafirishaji wa zao hilo jijini Dar es Salaam, Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alisema serikali imeanza kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha wakulima wanatafutiwa masoko ya uhakika.

"Leo tumetimiza jambo moja la kusafirisha parachichi kuelekea India ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Rais Samia. Lakini pia hii yote imetekelezwa ikiwa ni uhusiano mzuri kati ya Tanzania na India, lakini pia viongozi wa nchi hizo kukubaliana kusafirisha bidhaa hii," alisema Mavunde.

Mavunde alisema Novemba 25, mwaka jana viongozi wa serikali za Tanzania na India walikutana na kufanya mazungumzo ya namna bora ya kusafirisha zao hilo.

Alisema baada ya pande mbili kufikia muafaka, Idara ya Afya ya Mimea India ilitoa tangazo maalumu lililokuwa likitoa ruhusa kwa Watanzania kuanza kusafirisha parachichi kuelekea India.

"Leo tani zaidi ya mbili zinasafirishwa, sasa wakulima waanze kulima kwa tija ili tusafirishe bidhaa nyingi zaidi na bora, Tanzania tunazalisha tani 40,000 za maparachichi kwa mwaka lakini uwezo wa kusafirisha ni tani 9,000,' alisema.

Kwa mujiobu wa Mavunde, kwa sasa Wizara ya Kilimo iko katika maandalizi ya kuanzisha kituo maalumu cha kupokea parachichi kutoka kwa wakulima, ambacho kitakuwa na kazi ya kuchambua parachichi na kuziweka katika ubora kisha kusafirishwa kwenda nchi mbalimbali.

"Tunataka parachichi zetu zisomeke zinatoka Tanzania. Katika mazao ya mboga parachichi tunaipa kipaumbele cha kwanza, hivyo wakulima wajitokeze kwa wingi katika kulima," alisema Mavunde.

Mfanyabiashara aliyekuwa akisafirisha parachichi hizo, Sameer Gupta, alisema alianza mchakato wa kuomba ridhaa ya kusafirisha bidhaa hiyo tangu mwaka 2018.

Alisema kusafirishwa kwa parachichi kutoka Tanzania kwenda India kutaongeza mapato na kuinua uchumi wa Tanzania sambamba na kuitangaza kimataifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema; "Tumejitahidi kwa miaka mitatu kupata mzigo mkubwa kama huu. Tukienda India huwa tunarudi na mzigo wa tani nane hadi 12, lakini tunapokwenda tunakuwa na mzigo mdogo sana"

Matindi alisema ATCL iliangalia soko la India linataka nini na kubaini kwamba parachichi ndiyo zao lenye soko kubwa.

Alisema shehena hiyo ni ya pili kusafirishwa na ATCL na kwamba katika kipindi cha Januari wanatarajia kusafirisha tani 20 kwenda India.

# Kampuni yawasaka wanaoghushi bidhaa zake

**Na Mwandishi Wetu**

Kampuni ya Grace Products, maarufu kama 'Zoa Zoa' imeingia mitaani nchi nzima kwa lengo la kuwasaka wafanyabiashara wasio waaminifu ambao wamekuwa wakitengeneza sabuni duni na kuzihifadhi kwenye makasha yanayoonyesha zimetolewa na kampuni hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Grace Products, Dk. Elizabeth Kilili, alisema watu hao wasio waaminifu wamekuwa wakitengeneza sabuni bandia za Zoa Zoa Manjano na kuziingiza sokoni.

Dk. Kilili alisema wameshawakamata watuhumiwa kadhaa na kuwafikisha kwenye mikono ya sheria kwa taratibu zingine huku wengine wakiingia mitini baada ya kusikia oparesheni hiyo kali na ya kimkakati.

"Naomba niwaambie wateja wetu na Watanzania, ukimkuta mtu anauza sabuni zetu za Zoa Zoa Manjano, ili kuitambua kama ni feki au ndiyo yenyewe, gusa lile neno Zoa Zoa kwenye boksi. Kama ni feki utaona halina mwinuko, kama ni orijino, lina mwinuko ukigusa.

"Hata ile lebo ya Grace nayo ina mwinuko wakati feki hazina hali hiyo. Lakini pia niwaambie wale wanaoendelea au kuwaza kufanya magumashi ya sabuni zetu kuacha mara moja kwani oparesheni yetu siyo ya wazi." alimaliza kusema Dk. Elizabeth.




Rais wa Taasisi ya Al- Hikma, Sheikh Sharif Abdulqadir Alhdal (wa pili kushoto), akiongoza dua maalumu ya kuliombea Taifa amani, iliyoandaliwa na taasisi hiyo, Temeke, mkoani Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa Taasisi hiyo, Sheikh, Nurdeen Kishik. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tiketi za mwendokasi sasa kwa simu

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), imeanzisha mfumo mpya unaowawezesha abiria kukata tiketi kwa kutumia simu zao za mkononi lengo ikiwa ni kupunguza msongamano kwenye vituo vya mabasi.

Ofisa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa DART, Deus Felix, alisema hayo juzi wakati akizungumza kwenye semina ya siku moja kwa wahariri na waandishi wa habari iliyoandaliwa na wakala kwa kushirikiana na Jukwaa la Wahariri (TEF).

Felix alisema kupitia mfumo huo uitwao Dar City Navigator, abiria sasa watakata tiketi zao kabla ya kufika kwenye vituo vya mwendokasi hali ambayo itasaidia kupunguza foleni.

Alisema mfumo huo ulianza kutumika hivi karibuni na bado haujafahamika kwa abiria walio wengi hivyo alitoa wito kwa wananchi kujifunza kutumia mfumo huo mpya ili kwenda na wakati.

"Badala ya kwenda kununua tiketi kituoni sasa abiria anaweza kununua tiketi popote alipo anachotakiwa kufanya ni kupakua App ya Dar City Navigator ambayo inapatikana kwenye 'Google Playstore' kisha atakuta sehemu ya kupata tiketi. Akibonyeza ataingiza namba yake ya simu na hapo atakuwa tayari kununua tiketi yake," alisema.

Ofisa huyo alisema mfumo huo pia umetengenezwa kwa ajili ya kuwawezesha abiria kupata taarifa mbalimbali kutoka kwa wakala na kuripoti changamoto mbalimbali wanazozipata ili zipatiwe ufumbuzi.

"Tiketi utanunua kwa kuchagua sehemu utakayopandia na sehemu utakayoshukia lakini cha muhimu sana ni sehemu utakayopandia kwasababu sehemu utakayopandia ndiko utaruhusiwa kuingia na hiyo tiketi. 'Mfano kama unasafiri kutoka Kimara utachagua sehemu ya kupandia kwa kuandika Kimara na tiketi hiyo itakuwa na uhai wa saa tatu ndipo itaisha muda wake wa matumizi tunawakaribisha abiria wetu watumie mfumo huu mpya kwani uwasaidia kuepuka msongamano kwenye vituo vyetu," alisema

Kwa sasa, alisema mfumo huo mpya unatumika kwenye vituo 20 na mipango inaendelea kuhakikisha unawekwa kwenye vituo vyote 33 ili kuondokana kabisa na mfumo wa zamani wa kupanga foleni kwaajili ya kununua tiketi.

Kwenye semina hiyo wahariri na waandishi wa habari waliishauri DART kufanya maboresho mbalimbali ikiwemo kuweka watu watakaosimamia abiria wakati wa kupanda na kushuka kwenye mabasi hayo.

Mmoja wa wahariri, Tausi Mbowe, alisema kwenye baadhi ya vituo kumekuwa na utaratibu mbovu wakati wa kupanda ambapo abiria wamekuwa wakisongamana hali ambayo inakatisha tamaa watu wanaotaka kutumia usafiri huo.

"Kuna wakati mtu unatamani kabisa uache gari lako upande mwendo kasi kuwahi mjini lakini ile hali ya kugombania mlangoni wakati wa kuingia inakatisha tamaa watu wengi kutumia usafiri huu tafuteni watu wa kusimamia utaratibu ili usafiri uwe na hadhi si vurugu kama tunazoona," alisema.

# Walengwa TASAF wafurahia malipo kielektroniki

**Na Elizabeth Zaya,** HANDENI

WALENGWA wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (PSSN II), unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wamesema kuanza kulipwa pesa zao kupitia mfumo wa kielektroniki, kumewapunguzia lawama kwa watu pamoja na matumizi mabaya ya pesa hizo.

Wakizungumza juzi wilayani hapa, walisema awali kabla ya kuanza kutumika mfumo huo na kwenda kupanga foleni kusubiri malipo hayo ofisini ilikuwa inawaletea lawama hususani pale wanapokuwa wamekopeshwa na watu.

"Mwanzoni wakati tunapokea pesa zetu za TASAF ofisini, hali ilikuwa mbaya kwani wakati mwingine unasubiri malipo na wale wanaokudai kama uliwakopa, wanakusubiri hapo hapo. Kwa hiyo ukipewa tu unajikuta imeisha. Hata kama ulipanga uwalipe kidogo kidogo, lakini wengine wakiona mnalipwa hawakubali, wanalazimisha uwalipe yote.

"Lakini kwa sasa ukipokea hakuna hata anayejua. Ni wewe tu na simu yako, kwa hiyo inaleta hata utulivu wa kujipangia malengo na namna ya kuitumia kwenye vipaumbele vyako. Hata kama una deni unalipa kidogo na si kwa kusimamiwa kama kipindi cha nyuma, "alisema Hadija Ngadada, mlengwa kutoka Kijiji cha Kwakivesa.

Wanufaika hao pia walisema mfumo wa kupokea pesa mkononi ulikuwa unachangia kushawishika kuzitumia kwa haraka katika mambo yasiyo na maana bila mpangilio.

"Kwa hiyo wakati mwingine hata watoto walikuwa wakiona umepokea pesa zako na umezishika mkononi, wanaanza kukushawishi upitie kununua nyama ili wapike hata pilau wajichane na unakubali kweli na mwisho wa siku mnaimaliza mara moja tu," alisema Ngadala.

"Lakini kwa kutumia mfumo huu wa kulipwa kwa simu kielektroniki, pesa unatunza akiba na kuitumia tu kwa mambo ya maana," alisema.

Rahma Hussein, Mlengwa kutoka kijiji cha Msasa Shule, alisema malipo ya mfumo wa kielektroniki yamemsaidia kuwa na nidhamu ya kutunza pesa mpaka pale anapokuwa na matumizi ya msingi ndio huitoa kwenye simu tofauti na ilivyokuwa awali wakati akipokea mkononi moja kwa moja.

Kwa mujibu wa TASAF, mfumo wa malipo ya pesa kwa walengwa kupitia mfumo wa kielektroniki umeanza kutumika kwa walengwa hao kwa baadhi ya maeneo na kwamba lengo ni kuutumia nchi nzima.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu itolewe kukomesha mauaji ya wivu wa mapenzi

**KWA** takriban wiki nzima, vyombo mbalimbali vya habari nchini, vimeripoti taarifa mbalimbali kuhusu vifo vya watu hasa vinavyotokana na mauaji ya kikatili, baadhi yakidaiwa kuwa sababu ni wivu wa kimapenzi na imani za kishirikina.

Miongoni mwa vifo hivyo ni kile kilichotokea Arumeru mkoani Arusha ambacho kinadaiwa kimesababishwa na mwanaume kumuua mpenzi wake ambaye ni mke wa mtu akimtuhumu kutoa ujauzito wake. Mwanaume huyo, ambaye sasa anashikiliwa na polisi, anadaiwa alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke huyo, hali iliyosababisha kupeana ujauzito na hatimaye mwanamama akadaiwa kuutoa.

Kifo kingine ni kile kilichoripotiwa leo kutoka Songea mkoani Ruvuma cha mwalimu mstaafu kudaiwa kuuawa kwa sababu ya wivu wa kimapenzi. Taarifa za polisi zinaeleza kuwa mwalimu huyo aliyestaafu takriban miaka minne iliyopita alikuwa na uhusiano wa kimapenzi na mwanamke ambaye pia alikuwa na uhusiano pia na mwanaume mwingine.

Mbali na matukio hayo ya vifo pia kuna taarifa kutoka mkoani Singida kuwa mwili wa mtoto mwenye umri wa mwaka na mwezi mmoja umefukuliwa na watu wasiojulikana kisha kutokomea nao kusikojulikana. Mwili huo umepatikana siku chache baadaye ukielea kisimani.

Tukio lingine la mauaji linalodaiwa kusababishwa na imani za kishirikina ni lile la mkoani Mbeya ambalo askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) alidaiwa kumuua baba yake mzazi kwa tuhuma kwamba ndiye aliyekuwa akifanya mambo yake 'yasimnyookee'.

Kutokana na kuibuka kwa wimbi la vifo hivyo, baadhi ya wataalamu wametaja sababu kadhaa zinazofanya kuwapo kwayo, ushirikina ukiwamo. Imani hizo ambazo zimekuwapo kwa muda mrefu zimechangia kwa kiasi kikubwa mauaji ya wazee na vikongwe.

Matukio ya aina hiyo, husussan ya vikongwe, yalishamiri katika miaka ya 2000 hadi 2010 katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kutokana na ramli chonganishi kwamba baadhi ya vikongwe wanawaua watoto na wajukuu zao.

Kutokana na kushamiri huko, ilianzishwa kampeni maalumu iliyoshirikisha viongozi wa serikali, wanaharakati, washirika wa maendeleo , viongozi wa dini na jamii kwa ujumla. Kampeni hiyo, iliyoambatana na elimu kwa jamii, ilisaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza mauaji hayo.

Hata hivyo, wimbi hilo limeibuka upya lakini kubwa likiwa la mauaji ya wapenzi na wenzi huku sababu kubwa ikielezwa kuwa ni wivu wa mapenzi. Wakati sasa umefika elimu kuanza kutolewa kwa jamii ili kutokomeza vitendo hivyo ambavyo sasa vimeanza kuwa kama dondandugu.

Ni imani kwamba kama elimu itatolewa ipasavyo kuanzia ngazi ya shule za msingi huku viongozi wa mila na wale wa kidini wakichukua hatua kwa nafasi zao, jambo hilo linaweza kupungua na hatimaye jamii ikaishi kwa amani na usalama.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kashfa ya rushwa trafiki ni bora kusoma alama za nyakati

Na Sabato Kasika

**ASKARI** wawili wa Kikosi cha Usalama Barabarani wanadaiwa kukamatwa kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa, na tayari kashfa hiyo imefika kwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi , Hamad Yussuf Masauni.

Kwa mujibu wa Waziri Masauni, watuhumiwa hao ni wa mikoa ya Iringa na Kilimanjaro, na kwamba kukamatwa kwao kunatokana na ushirikiano kati ya vyombo husika na wananchi ambao hutoa taarifa za vitendo hivyo.

Askari hao wamenaswa huku kukiwa na wito wa mara kwa mara kutoka kwa Rais Samia Suluhu Hassan wa kuwataka askari wa kikosi hicho kuwa na lugha nzuri kwa raia na kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Rais amewahi kusema baadhi ya askari hao wana vitendo visivyofaa, ikiwamo kusimamisha magari na kuwataka madereva kuwapa fedha, vitendo ambavyo vinakwenda kinyume na maadili ya kazi yao.

Ni wakati akifungua mafunzo ya kozi ya maofisa wa Jeshi la Polisi, jijini Dar es Salaam mwaka jana, na kukemea vitendo hivyo huku akiwataka wafanye kazi yao inavyotakiwa bila kumuonea mtu.

Si mara ya kwanza Rais Samia kukemea vitendo hivyo, kwani kuna wakati aliwahi kusema, ana clip zinazoonyesha askari hao wakipokea fedha na kuwataka waache aibu hiyo.

Kwa kauli hiyo, ilitosha kuwafanya kusoma ishara za nyakati na kujiweka pembeni ili kuwa salama dhidi ya vitendo hivyo ambavyo Rais alisema ni vya aibu na vinakwenda kinyume na maadili ya kazi yao.

Kimsingi, alichosema Rais, kilitosha kuwafanya kuwa makini na kujiweka kando, kwani katika mazingira hayo, wanaweza kuwapo wenzao ambao 'wanawachomea utambi', au abiria ama madereva wa magari.

Ingekuwa ni vyema askari wengine kujifunza kutokana na makosa kwa kutojiingiza katika mchezo huo, kwani kama watajiingiza katika vitendo hivyo, wajue kuwa wanafuatiliwa na watu wengi.

Katika usafiri wa daladala, baadhi ya abiria hujiuliza kuwa kondakta anahusikaje kama gari lina tatizo? Swali hilo linatokana na kwamba, trafiki wanapoisimamisha, kondakta hushuka na kuwafuata nyuma ya gari.

Mbaya zaidi ni kwamba, kondakta anaporudi ndani ya gari huelezea kile alichoitiwa, hivyo kwa mazingira kama hayo, inaweza kuwa rahisi askari kunaswa iwapo hawataacha mtindo huo unaokemewa.

Ninaamini kuwa ni udhalilishaji kusikia kondakta au dereva wa daladala, bodaboda ama bajaj wakiwaita askari hao kuwa ni watu wa njaa. Ninaona kama jina hilo ni la kuwadhalilisha mbele ya umma.

Ikumbukwe kuwa katika usafiri wa umma huwa kuna watu mbalimbali wakiwamo hata wale ambao wanaweza kuchukua taarifa za vitendo hivyo na kuzifikisha mahali husika na hivyo askari kujikuta katika matatizo.

Katika Kiswahili, kuna msemo kwamba; 'Ukiona mwenzio ananyolewa, na wewe zako tia maji', hivyo hatua ya kukamatwa kwa askari hao kwa tuhuma za rushwa, iwaamshe wenzao kuepuka kuingia mtegoni.

Jambo la kuzingatia ni kwamba, Rais ana vyanzo vingi vya habari, hivyo anapokemea vitendo hivyo, ni wazi atakuwa ana ushahidi wa kutosha kutoka katika vyanzo vyake vinavyomfikishia taarifa.

Wakati mwingine vyanzo hivyo vinaweza kuwa katika usafiri huo wa umma vikishuhudia vitendo vyote vinavyofanyika. Hivyo suala la kusoma ishara za nyakati ni la muhimu kuepuka kuingia mtegoni.

Tangu kuibuka kwa skendo hiyo, wameibuka watu wa kada mbalimbali wanaotoa ushauri wa kutaka askari wa kikosi hicho kujisahihisha ili kutokipaka matope kikosi hicho kutokana na tabia ya askari wachache.

Hatua hiyo inatokana na kile nilichoeleza kuwa katika usafiri wa umma, kuna watu mbalimbali na inawezekana wakawamo wanaomfikishia taarifa kiongozi wa nchi kuhusu vitendo vya baadhi ya askari hao.

Kwa maana hiyo, kauli ya awali aliyoitoa Rais kuhusu tuhuma za rushwa kwa baadhi ya trafiki, ingetosha kuwafanya wasome ishara za nyakati na kuepuka kuwa katika mazingira yanayoweza kuwaingiza katika tuhuma za rushwa.

## SAFU/MAKALA

### KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hongera Dk. Tulia, tunaomba uthibitishe kuwa Spika Bora



Na Pascal Mayalla

**Wenzetu wazungu wanaita, 'endorsement', hivyo leo nafanya 'endorsement' yangu kumpata Spika Bora kwa kutumia udhaifu wa Spika aliyepita na makosa ya msaidizi wake huku nikipendekeza spika bora.**

LEO ni mwendelezo wa mada ya wiki iliyopita kuhusu Spika Bora na Bora Spika. Niliwaomba chama tawala-Chama Cha Mapinduzi (CCM) kituteulie Spika Bora. Nilisema hivyo kwa sababu mteule wa CCM akishateuliwa na chama chake, huyo ndiye Spika.

Japo kwa sasa jina lililopendekezwa na CCM ni moja la Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, kikao cha Wabunge wa CCM kitakamilisha tu taratibu na uchaguzi wa Spika utakaofanywa na Bunge. Nikirejea kwenye mada yangu, je, chaguo hili ndiye Spika Bora?.

Naomba kuanza kwa kuwaletea maono niliyoyaona mwaka 2019 na kuyaandika katika mtandao maarufu wa Jamii Forums chini ya kichwa cha habari "Voices From Within: Nimesikia sauti, Spika Ndugai Ataukatizia Uspika, Dk. Tulia Ackson ndiye Spika ajaye!" Japo siku zote Nabii hakubaliki nyumbani, nalijua hili Job Ndugai kuukatiza uspika kwa sasa litabezwa, ila litakapotokea ndipo tutaelewana. Ndivyo nilivyoandika.

Haya ni maono ya unabii na si utabiri. Unasikia tu sauti inakwambia jambo fulani bila kuambiwa sababu na huwezi kuuliza, hivyo nami naomba kuwaeleza tu sauti niliyosikia na naomba msiniulize kitu kwa sababu si mimi ni sauti.

Pia niliandika "Leo nilikuwa naangalia Bunge la Marekani (The Congress) linavyomshughulikia rais wa Marekani, Donald Trump, ambapo azimio la kumshtaki kwenye Bazara la Senate limepitishwa, japo kule Senate itakuwa ngumu kwa azimio hilo kupata ile theluthi mbili ya kumwondoa ila kumshitaki tu Rais ni hatua kubwa."

Kuna mchangiaji mmoja akasema hata Tanzania ikithibitishwa Rais amevunja anaweza kushtakiwa? Ndipo nikauliza ni Bunge lipi hilo la kumshtaki Rais?. Nikauliza kama ni Bunge hili hili la Ndugai au ni Bunge lijalo? ndipo mara ghafla nikasikia 'voice from within' ikiniambia kuwa Spika Ndugai hataendelea kuwa Spika, Spika ajaye ni DK. Tulia Ackson.

Sauti hiyo ikaniambia japo Ndugai atakuwa anatamani sana kuendelea kuwa Spika, hatakuwa kwa sababu fulani (japo sauti hiyo imenieleza hizo sababu za kwa nini hataendelea kuwa Spika Bunge lijalo, si lazima kusema kila unachosikia kwa sababu wakati mwingine kila unachosikia 'from within' ni sauti kutoka kwa Mungu au ni maono. Sauti zingine ni za shetani tu na si za Mungu, kama zilivyo ndoto zingine, ni za shetani. Ukisikia sauti ukahisi inaweza isiwe Mungu au ukiota ndoto ya jambo la ajabu, usiliseme au usiiseme!.

Tangu Samuel Sitta, mwenendo unaonyesha kwamba kiti cha Spika ni muhula mmoja wa miaka mitano tu na muda huo ukiisha, Naibu Spika ndiye anavaa joho la uspika. Baada ya Sitta alichukua Anne Makinda ambaye alikuwa naibu wa Sitta. Makinda alipomaliza miaka mitano akachukua Ndugai ambaye naye alikuwa naibu kwake na sasa Dk. Tulia, ambaye mpaka sasa ni naibu spika, anachukua kutoka kwa Ndugai.

**"Voices From Within" ni Nini?**

Hizi ni sauti kutoka ndani yako, ndani ya moyo wako, ndani ya nafsi yako, ndani ya dhamira yako. Yaani unasikia tu sauti fulani ikikuambia kitu kutoka ndani mwako. Sauti hiyo inaitwa moyo, Kiingereza wanaita 'conscious' au kwa Kiswahili dhamira.

Mara nyingi hutokea unapotaka kufanya jambo fulani, unajisikia kama kusitasita au unapotaka kusafiri unajisikia kama roho inakataa, usilazimishe.

Hicho unachosikia ndiyo 'conscious' yenyewe, ni sauti ya Mungu iliyo ndani yako, ama inakupa maono fulani, taarifa fulani, kukuonya usifanye jambo fulani au kukuonyesha jambo fulani litakuja kutokea baadaye.

'Voices from Within' si utabiri wala ubashiri. Ni maono tu na ndio ukweli halisi lakini si lazima yatokee. Unapotaka kufanya jambo, lile 'voice from within' inayokuambia hapana na kwa upole, ndiyo sauti ya Mungu na ile sauti kubwa inayokushawishi kwa kelele ikukwambia fanya tu, kubali tu, nenda tu, ndiyo sauti ya shetani. Si kila kitu unachosikia ni lazima kitokee, vingine havitokei lakini vikitokea ndipo unakumbuka.

Lakini jambo lingine la kujiuliza ni je, maono ni lazima usikie wewe? Vipi akisikia mwingine? Maono ni utaratibu wa Mungu aliyeko ndani yako kukuonya, Mungu anaweza kuongea na wewe kupitia fikra mawazo, maneno au kwa matendo kupitia ishara fulani au hata kupitia kwa wengine.

Ni kama Mungu alivyonena kwa vinywa vya manabii.

Wiki iliyopita nilisema Spika aliyetangulia hakuwa Spika Bora bali ni Bora Spika, hivyo ikitegemewa Naibu wake pia atakuwa ni Bora Spika. Pamoja na hayo, ili athibitishe kuwa ni Spika Bora kuna mambo mawili ya kufanya.

Kwanza, tumpe kitu kinachoitwa 'the benefits of doubt' kwamba japo alikuwa Naibu Spika chini ya Bora Spika, akitegemewa na yeye atakuwa Bora Spika, ana fursa na anaweza kabisa kuwa Spika Bora. Pili, tuahidi kumpatia kila aina ya ushirikiano Spika Mpya Dk. Tulia Ackson ili awe Spika Bora.

**Hongera Dk. Tulia, Mungu Ibariki Tanzania.**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Buku tano za kiwi lazima zitutokee puani



Na Joseph Kulangwa

**Kwa nini nayasema haya? Ni kwamba juzikati hapa, afande wangu mmoja alidakwa Iringa akiwa amesokomeza buku buku na buku mbili mbili kunako maeneo baada ya kuzikusanya barabarani kutoka kwa Watanzania wenzake, ili mradi wanasafiri kwa barabara.**

ILIKUWA zamani, pengine na sasa iko hivyo kwamba mkubwa alipokuwa akiachwa na mtoto nyumbani, hususan mtoto mdogo, alipewa jukumu la kumlisha chakula au kumnywesha, kama si maziwa basi uji.

Hilo lilikuwa jukumu la mtu mkubwa ili mradi halingani na kitoto alichoachwa nacho nyumbani kuhakikisha kinakunywa au kula na kushiba ili kisisumbue kwa njaa kwani mtoto daima hawezi kuhimili njaa.

Ilipotokea kuwa mtu mzima au mkubwa ameshindwa jukumu hilo badala ya kumnywesha mtoto maziwa au uji au kumpa chakula na akafakamia yeye, kwa kweli adhabu ilistahili iwe ya viboko na kutengwa.

Hiyo haikuwa tofauti na hivi sasa ambapo mtu anapewa madaraka badala ya kuyatumia vyema, anafanya anavyojua kwa kukengeuka na kushindwa kuwatumikia waliompa madaraka hayo, akitumikia maslahi yake binafsi na si ya umma.

Mtu mzima kufakamia maziwa au uji wa mtoto achilia mbali chakula chake, ni ukosefu na utovu wa maadili. Ni kushindwa kuvumilia njaa na kuacha mtoto asishibe na kulala kama inavyotakiwa kuwa katika familia iwayo yote ile.

Kwa nini nayasema haya? Ni kwamba juzikati hapa, afande wangu mmoja alidakwa Iringa akiwa amesokomeza buku buku na buku mbili mbili kunako maeneo baada ya kuzikusanya barabarani kutoka kwa Watanzania wenzake, ili mradi wanasafiri kwa barabara.

Huyu ni ndugu trafiki ambaye alishajiridhisha kuwa hakuna kwingine kwa kujipatia kipato, isipokuwa kusanya kwa madereva, utingo na makondakta wapitao na zao barabarani na yeye kuwa mtoza ushuru asiye rasmi.

Najua si wengi hawa katika Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, ni wachache tu wasio na maadili ambao kwa sababu zao na kwa kipaumbele cha njaa, wameona ni bora kutinga barabarani mchana kutwa na kugeuza barabara ATM yao.

Ni hawa ambao kwa sababu za kusaka eti 'buku tano za kiwi', wanaona kila senti ya dereva wa basi, lori au gari dogo, ni halali yake na ili upite salama huna budi kuingia mfukoni na kugawana naye ulichonacho.

Hawaamini kwamba upolisi ni wito kama ulivyo utawa, ualimu nakadhalika. Wanadhani kuingia Polisi na hasa Trafiki basi ni mwanzo wa kuuona ufalme wa njuluku, unajipatia bila jasho, unakula kwa jasho la mwingine. Haifai kabisa.

Unashangaa unapokuwa barabarani kukuta ndugu zetu hawa, baadhi yao wamejikusanya wakiweka magari pembeni na badala ya kutoa elimu, wanatoa maagizo ya toa kitu kidogo kwa maslahi yao madogo. Nasema si wote na wala si wengi bali ni walioingia huko kwa ajili ya kusaka tonge wakila kwa urefu wa kamba zao mpaka kuvimbiwa.

Hujiuliza sana tu, hivi kwa nini polisi ndugu zetu hawa, saa zote wajipange barabarani kusimamisha magari kana kwamba wamesikia kuna mhalifu anapita njia hiyo, hivyo kila gari lipekuliwe? Kwa nini wasisubiri kusikia gari fulani limesababisha kadhia hii ndipo walivizie kulikamata?

Ni kweli usalama barabarani ni muhimu sana hasa kutokana na baadhi ya madereva kichwa ngumu wasiotaka kufuata sheria za barabarani, wasiotaka kutii bila shuruti, hao ni kibano tu hakuna lingine, lakini si kila gari lipitalo barabarani lisakamwe.

Hivi kwa mfano, uko barabarani una haraka zako na huko uendako, ingawa unafuata kila kilichoagizwa barabarani, kwamba unaangalia mwendo unaotakiwa na unapakia mzigo unaotakiwa au abiria wanaotakiwa, lakini unafika mahali unapigwa mkono kuulizwa leseni tu na kama unayo unaambiwa ondoka!

Lakini mwingine mathalan anakusimamisha na kukuuliza unatoka wapi na unakwenda wapi. Humu humu Tanzania, kana kwamba u mgeni au unavuka mpaka? Ya nini? Subiri kama ninakosa basi tushughulikiane, lakini si kuniuliza unatoka au unakwenda wapi au unakagua leseni wakati sijapata tatizo lolote.

Hii yote inatoa mwanya wa watu kuomba buku moja buku mbili na matokeo yake ndipo kukutwa zimesondekwa kunako kofia, nguo ya ndani na kwingineko na kusababisha mtafaruku na kudhalilishana tu kama tukio hii la juzi.

Tuheshimu basi rangi nyeupe tunayovaa ambayo ni alama na ishara ya amani na roho safi! Tuheshimu Jeshi na nchi yetu basi!

**Duh alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Mliotoswa uspika msiweke kinyongo kwa chama tawala



Na Thobias Mwanakatwe

JANUARI 9, mwaka huu, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kilitangaza ratiba ya kuchukua na kurejesha fomu za kumpata mwanachama atakayewakilisha chama kugombea nafasi ya Spika wa Bunge la Tanzania.

CCM ilitangaza mchakato huo kutokana na aliyekuwa Spika, Job Ndugai, kujiuzulu nafasi hiyo Januari 6, mwaka huu. Mchakato huo wa kuchukua fomu ulianza rasmi Januari 10 na kufikia tamati Januari 15.

Hadi dirisha la kuchukua na kurejesha fomu linafungwa, wanachama 71 walijitokeza.

Kujitokeza kwa idadi kubwa ya wanachama, kulizua mjadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii huku baadhi ya watu wakifikia hatua ya kutaja wanaofaa kumrithi Ndugai kulingana na vigezo walivyoviona.

Mjadala ulikuwa mkali kwa sababu miongoni mwa waliochukua fomu walikuwapo vigogo ambao walipewa nafasi kubwa za kupitishwa na chama kuwania nafasi hiyo muhimu kwa mustakabali wa taifa hili.

Kwa uchache, baadhi ya wana-CCM waliochukua fomu ni Mussa Azzan Zungu (Mbunge wa Ilala), Dk Tulia Ackson (Mbeya Mjini), Luhaga Mpina (Kisesa), Stella Manyanya (Nyasa), Godwin Kunambi (Mlimba) na Joseph Musukuma (Geita Vijijini), Andrew Change, Goodluck ole Medeye,Sophia Simba, Dk Thomas Kashililah, Ezekiel Maige, Goodluck Mlinga na Norman Sigalla.

Lakini wakati wananchi wakitoa maoni yao kwenye mitandao ya kijamii, walisahau kuwa CCM ni chama ambacho kinazingatia sana demokrasia na kimejiwekea utaratibu mzuri wa kuwapata viongozi.

Utaratibu mzuri ambao CCM imejiwekea ndio uliotumika Januari 20 pale Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa, ilipoamua kupitisha jina la Dk Tulia Akson pekee kuwa mgombea wa kiti cha Spika.

Shaka akizungumza na wanahabari jijini Dodoma alisema CCM imeamua kupeleka jina moja tu badala ya utaratibu uliozoeleka wa kupeleka majina yasiyozidi matatu kwenye kamati ya wabunge.

Dk. Tulia anakuwa mwanamke wa pili kuwa Spika kama atachaguliwa na wabunge. Wa kwanza alikuwa Anne Makinda aliyeshika nafasi hiyo mwaka 2010 hadi 2015.

Mbali na CCM, chama cha upinzani cha Alliance for Democratic Change (ADC) nacho kimefungua mchakato huo na mwanachama wake Maimuna Kassim amekuwa wa kwanza kuchukua fomu za kuomba kuteuliwa kukiwakilisha katika uchaguzi wa nafasi ya Spika.

Sasa nije upande wa wanachama wa CCM 70 ambao hawakuteuliwa na chama kuwania uspika. Imekuwa mazoea wakati wa uchaguzi mbalimbali wanajitokeza wanachama wengi kuwania nafasi fulani lakini mwisho wa siku chama ndicho chenye mamlaka ya kuteua jina moja.

Ndani ya chama hiki tawala pamoja na utaratibu wa kupata viongozi wake kuwa wazi, naweza kusema kuliko vyama vingine, baadhi ya wanachama wanaposhindwa kuteuliwa wanaweka kinyongo kwa chama.

Naomba mlioachwa kwenye uspika msitengeneze makundi na kuweka kinyongo kwa chama kwa sababu wakati mnakwenda kuchukua fomu ya kuomba kuteuliwa, mlifahamu wazi kuwa nafasi inayotafutwa ni moja, hivyo haiwezekani mkateuliwa wote.

Watazamaji na wananchi tunawashukru kwa kutumia demokrasia yenu kuchukua fomu lakini chonde chonde msiweke kinyongo. Kumbukeni Mungu ndiye anatoa uongozi kwa hiyo kama mmekosa leo nina imani mtapata kesho.

Huu utamaduni wa kununa baada kushindwa kuteuliwa, umeshapitwa na wakati na nitawashangaa mliochukua fomu kama mtanuna kisa mmeachwa wakati mnafahamu kuwa mlipoenda kuchukua fomu ilikuwa ni kama bahati nasibu kupata au kukosa.

Mlioachwa kuwania uspika mfahamu kuwa CCM kulinganisha na kizazi cha vyama vyenzake vya ukombozi vilivyotimuliwa madarakani imekuwa ina demokrasia pana ya ndani ya chama na mifumo madhubuti ya kutatua migogoro na hivyo kukiwezesha kuhimili misukosuko.

Baada ya Rais wa kwanza, Julius Nyerere kung'atuka, kumekuwa na kupokezana madaraka kwa marais watano mpaka sasa.

Ukiangalia vyama vya ukombozi katika nchi nyingine, vingi viliponzwa na ukosefu wa demokrasia na uwezo mdogo wa kushughulikia migogoro ya ndani. Mfano KANU iliponzwa na Rais Daniel Arap Moi aliyejaribu kuwachagulia Wakenya mrithi. Naye Dk. Kamuzu Banda wa Malawi alishajikabidhi uenyekiti wa chama na urais wa maisha wa nchi yake. Wawili hawa walipalilia uasi ndani ya vyama vyao.

Kwa msingi huo mliachwa kuteuliwa kuwania uspika msinune acheni demokrasia iendelee kutawala ndani ya CCM.

**Kwa maoni ya ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@yahoo.com**

**MUNGU IBARIKI TANZANIA MUNGU LIBARIKI BUNGE LA TANZANIA**

## DARASA LA NDOA

# NAMNA YA KUISHI NA WATUMISHI WA NDANI KATIKA FAMILIA -2



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

KATIKA sehemu ya kwanza ya makala hii, tuliona kwamba familia nyingi hukutana na changamoto nyingi za namna ya kuishi na watumishi wa ndani huku baadhi yao wakijisikia watumwa badala ya kuwa sehemu ya familia wanazofanyia kazi. Wengi wao hujisikia kutumikishwa na kunyanyaswa kwa kufanya kazi zisizo zao na zilizo nje ya uwezo wao. Kipato wanachopata hakiendani na majukumu mengi ya kikazi waliyo nayo katika familia husika.

Pia watumishi wengi wa ndani hawapewi stahiki zinazolingana na majukumu yao katika familia nyingi wanazotumikia, tena baadhi yao hawalipwi kwa wakati. Pia wako ambao hawalipwi chochote kwa kisingizio cha mwajiri kuwa anamtunzia fedha zake.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watumishi wa ndani hawajitambui. Baadhi yao ni wajeuri, wavivu, si waaminifu, watovu wa nidhamu, watu wa manung'uniko, hawana shukrani kwa waajiri wao kutokana na makuzi katika familia walizotoka. Hatua hiyo imesababisha wanafamilia kuchukua tahadhari na kuwa makini wanapoishi na watumishi hawa.

Nini kifanyike kukabiliana na changamoto za watumishi wa ndani?

●Wanandoa wafahamu nafasi na wajibu wao. Uwapo na mtumishi wa ndani katika familia haimaanishi kuondoa nafasi na wajibu wa mume na mke katika ndoa. Kazi ni muhimu lakini isiwe sababu ya kutelekeza familia na majukumu ya kindoa. Wanandoa wawe na muda na nyumba zao na familia. Wapende kujishughulisha wawapo nyumbani ili wasiwe wageni katika nyumba zao.

●Ni muhimu kuwafahamu vizuri wale tunaowaruhusu kuishi nao katika nyumba zetu. Fahamu mahali na familia anayotoka, imani yake na historia yake. Changamoto ya kutokumfahamu mtu inakuwa kubwa na yenye madhara hasa pale inapozaa matukio ya ajabu na kutisha. Watu wengi wamelizwa na kuumizwa na watumishi wa ndani kwa sababu ya kutokuwafahamu vizuri mapema.

●Watumishi wa ndani waelekezwe majukumu yao kwani yale mwajiri anayotamani yafanyike, inawezekana mtumishi wake hayajui kutokana na mazingira na familia aliyotoka. Kumekuwa na changamoto kwa mtumishi wa ndani hasa pale anapokuwa hatambui vizuri majukumu yake katika familia husika. Ni muhimu sana watumishi waelekezwe na kuambiwa cha kufanya na jinsi ya kufanya (induction) na wapewe vitendea kazi. Kuelekeza lisiwe jambo la zoezi la siku moja tu, bali liwe endelevu mpaka pale utakapojiridhisha kuhusu ubora na utendaji wake ili kukidhi matarajio yako. Watumishi wa ndani wakumbushwe na kukosolewa kwa upole na upendo pale wanapokosea kuliko kutafuta makosa yao tu. Kinyume na hapo, mtumishi anaweza asikidhi matarajio ya mwajiri wake kwa sababu hajafundishwa na kuelekezwa yampasayo kufanya na mipaka yake.

●Wanafamilia wawe na mipaka na watumishi wao wa ndani. Suala la kutunza mipaka ni muhimu sana kwani linajenga na kutunza heshima na nidhamu. Watumishi wa ndani wasitumike kama watumwa na kuwa bidhaa, bali watambulike kuwa ni watu wanaostahili heshima. Utumishi wao ndani ya familia isiwe sababu ya kunyanyaswa na kuwafanyia vitendo vya ukatili. Watumishi hawa wanahitaji upendo na kuthaminiwa ili wawe na moyo wa kufanya kazi zao vizuri na kuleta tija.

●Wanafamilia wasibweteke. Pamoja na uwapo wa mtumishi wa ndani, wazazi na watoto wao wajishughulishe katika nyumba zao. Wazazi na watoto wasipojishughulisha na shughuli yoyote ya nyumbani, huu ni mwanzo wa kutengeneza kizazi kisichojitambua na kutokuwajibika katika maisha yao binafsi, familia na jamii kwa ujumla. Ni muhimu sana watoto wapate maarifa ya nyumbani ili baadaye wawe baraka kwa wazazi wenyewe na watu wengine.

●Watumishi wa ndani wapewe muda wa kupumzika kwani wao si vyuma, bali ni binadamu wanaochoka kama binadamu wengine. Watoto wafundishwe kuishi vizuri na kuwaheshimu watumishi wa ndani kwani ni wasaidizi wa wazazi wao katika utekelezaji wa majukumu ya nyumbani.

●Watumishi wa ndani ni binadamu wenye mahitaji kama binadamu wengine. Hivyo, wapewe ujira wao kwa wakati ili wawe na moyo wa kutekeleza majukumu yao vizuri na kujenga uhusiano mwema na waajiri wao. Ni muhimu kutambua jitihada na mchango wao katika familia na kuwatia moyo badala ya kuwakatisha tamaa kwa kauli mbaya zisizo na staha na matendo yasiyofaa.

●Watumishi wa ndani ni watu wenye hisia kama watu wengine. Wanafamilia wawathamini na kuonesha utu kwa watumishi hawa ili nao wapokee mema yao. Mtumishi anapokosea akosolewe na kusahihishwa kwa namna nzuri ya kufundisha na kuelekeza. Kinyume na hapo, hasira yake kwa kuhisi kutendewa isivyo, inaweza kumfanya alipize kisasi kwa kudhuru watoto ulio nao au wewe mwenyewe, kuharibu mali ulizo nazo na kutoroka.

●Watumishi wa ndani watimize wajibu wao ipasavyo na kuwa na bidii. Waishi kulingana na mazingira ya familia wanazofanyia kazi. Wawe waaminifu na kuthibitisha umuhimu wa uwapo wao katika familia walizopo. Uaminifu na utendaji mzuri wa kazi ndio utakaowabakiza kazini na kumhamasisha mwajiri kutenda mema na makubwa zaidi kwa ajili yao. Watumishi waoneshe shukrani kwa yale mema wanayotendewa na waajiri wao badala ya kulaumu kila kitu. Wawe na tabia njema, wajiheshimu na kuheshimu waajiri wao.

●Watumishi wa ndani wapewe muda wa kwenda kwenye nyumba za ibada kuabudu kadri ya imani ya mtu ili wakue kiroho na kiimani. Hii itasaidia sana katika kuwafanya kuwa baraka badala ya kuwa karaha katika familia walizopo. Watumishi hawa wanahitaji kutunzwa na kutendewa mema kama wanavyotendewa wanafamilia wengine.

Mwisho, watumishi wa ndani wanaweza kuwa lango la baraka au laana katika familia kutegemea na namna wanavyopatikana na jinsi familia zinavyoishi nao. Familia zitende wema kwa watumishi wa ndani bila kujali wao ni kina nani kwa sababu sisi sote ni binadamu na tu mali ya Mungu. Wema na utu wa mwajiri kwa mtumishi wake ni kichocheo cha furaha na utendaji wenye ufanisi.

**●Mch.Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

JANUARI 23, 2022

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

**FURAHIA LADHA**

**Juice ya Karoti, Tangawizi, Nanasi**




Ukurasa 14

## UREMBO:

VIKUKU

Pambo la kale linalodumazwa




## KATUNI


Ukurasa 16




# Mambo ya kuzingatia kabla ya kuuza nyumba

Ukurasa 15


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | D | E | N | G | E |
| ■ | U | ■ | ■ | E | ■ |
| A | K | A | ■ | R | ■ |
| ■ | A | ■ | P | E | A |
| ■ | N | ■ | ■ | Z | ■ |
| K | I | N | G | A | ■ |

## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | | | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | ■ | | ■ |
| ■ | | ■ | | | |
| ■ | | ■ | ■ | | ■ |
| | | | | | ■ |

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
DAU, AMA, TAMBI, JAZWA, WAKATI, JAMBIA

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

MTOTO Grace alikuwa akitembea juu ya sakafu ya marumaru kwa mwendo wa haraka, mama yake alimwangalia na huku akiwa na hofu asije akateleza na kuanguka chini.

Mama: Grace unakimbilia wapi, hujui kama unatembea kwenye marumaru?

Grace: Mama nakwenda kuchukua kitabu changu cha hadithi Juma ameniibia.

Mama: Lakini kuwa mwangalifu, usije ukaumia na mimi sina pesa ya kukupeleka hospitali.

Grace: Lakini mama kule shuleni mwalimu alitufundisha kwamba 'kuteleza si kuanguka', hivyo sina hofu.

Mama: Hapana mwanangu huo ni msemo tu alitaka kuwajenga muwe na ujasiri wa kufanya jambo ambalo awali umeshindwa.

SWALI
Taja aina tatu ya wanyama wa jamii ya swala wanaopatikana porini.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Ijue hatari ya mtu kufa ndani yake

KARIBU tena msomaji wangu tujumuike kwenye safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo tutaangalia hatari ya mtu kufa kunakoanzia ndani ya moyo wake.

Mwanadamu ni ndani na nje. Unapomwona mtu kwa nje, yaani kwa macho ya mwili ndivyo alivyo ndani yake. Ukimwona mtu anafanya vituko, shida haiko nje kwa jinsi unavyomwona, bali iko rohoni mwake.

Ukimwona mtu anampiga mtu mwingine, maana yake shida ya kumpiga haijaanzia nje, ilianzia ndani. Ndiyo maana nikasema kuna hatari ya mtu akafa ndani. Kwa mantiki hiyo, kifo cha ndani ni hatari zaidi kuliko kifo cha nje.

Kifo chochote hakianzii nje bali ndani. Ukiona mtu anakuwa na roho mbaya, anakuwa mjeuri, hiyo haianzii nje bali ndani.

Ukiona mtu mambo yake yanaharibika, kila anachoshika kinaharibika, hana mafanikio, hana matunda, hana kitu cha kuonyesha, huyu mtu hajaanza nje kwani kifo cha mambo yote hayo kimeanzia ndani yake.

Pengine kila akishika fedha hazikai, hiyo haianzi nje bali ndani yake. Unapoona biashara zako haziendi au ukiona maisha yako ni mabaya, anza kuchunguza ndani yako! Kila mtu anapaswa kujichunguza moyoni mwake kwamba, je, kupo salama?

Haiwezekani nje kukawa salama wakati ndani yako hakuna usalama. Siku zote mwonekano wako wa nje ni taswira ya ndani. Mtu anaweza kujifanya mzuri kwa nje lakini kwa ndani yake sivyo alivyo.

Ni muhimu mtu akatae kufa ndani. Huwezi kwenda zaidi ya ndani yako. Huwezi kufanikiwa zaidi ya ndani yako. Moyo wako ulivyo ndivyo yalivyo mafanikio yako, kadhalika na uzima wako!

Mtu anaweza akajifanya na kukuaminisha kile anachokisema kwa kukenua meno yote nje kwamba ni kweli kabisa. Lakini kumbe ndani ya moyo wake kunasema tofauti. Jiulize ndani yako kunaongea kitu gani?

Watu wengi sana ndani ya mioyo yao hakuna usalama. Ndio maana maisha hayapendezi, mambo yao hayaendi wala hawana maisha bora yenye amani wala mafanikio.

Mungu akauliza katika moja ya maandiko yake kwamba; Je! Chemchemi katika jito moja hutoa maji matamu na maji machungu? Hii ikimaanisha, moyo wa mtu mmoja unaweza kuwa mbaya na mzuri kwa wakati mmoja?

Ndani ya moyo wa mtu mmoja anaweza kutoa chuki na upendo? Ni kwa nini watu wengi sana wanasimama kisha wanaanguka. Wanaomba rehema Mungu awasamehe lakini wanarudia mabaya, masengenyo, ni kwa nini?

Ukweli ni kwamba ndani ya mioyo yao wameharibika. Nimesema ndani ya mtu haiwezekani vikatoka vitu viwili, yaani kwa wakati mmoja ukatoka upendo na chuki, hapana.

Nikaeleza pia kwamba kifo kinaanzia ndani na siyo nje. Utaona mtu anatembea barabarani, kumbe ndani yake kuna ugonjwa unaomtafuna taratibu hatimaye utamuua. Hii ikimaanisha kuwa nje ni matokeo ya ndani.

Kwa hiyo, unapoona mambo yako yanaharibika, mipango yako haiendi, unajitahidi sana kupambana lakini hutoboi. Ni kama mtu unayetaka kufanikiwa lakini hufanikiwi, jitafakari usibaki tu unashangaa.

Msomaji wangu, unapofikia hatua kama hiyo, chunguza ndani yako, je, upo sawasawa? Unaweza kuwadanganya wanadamu lakini huwezi kumdanganya Mungu.

Mungu ni mchunguzi wa haki. Yeye anakujua mwanzo hadi mwisho wako. Ndio maana anakuuliza, je, ndani ya chemchem moja kunawezaje kutoka maji matamu na maji machungu? Hiyo haiwezekani kwa sababu yakitoka matamu yale machungu hayapo!

Watu wengi sana wana roho mbili zinazofanya kazi kwa wakati mmoja. Jiulize ni kwa nini watu wanalia mbele za Mungu, kisha wanarudia machafu?

Kwa nini unamuomboleza Mungu kwa matatizo unayopitia lakini ukitoka hapo ni kama vile haujaomboleza?

Je, hujui kwamba unamdhihaki Mungu wakati hadhihakiwi wala hajaribiwi? Kwa nini umlaumu kwamba hakujibu maombi yako wakati shida iko ndani yako? Jichunguze utagundua tatizo linaanzia kwako mwenyewe!

Mungu ni Mungu wa kanuni. Lazima ujitafakari na kujiuliza ni kwa nini umeomba rehema, kwanini umemlilia Mungu lakini hujibiwi. Unapaswa kutubu dhambi na wala usizirudie tena. Maisha Ndivyo Yalivyo.

***Msomaji wangu, bila shaka, umejifunza jambo hapo. Fuatilia sehemu ya pili ya mada hii wiki ijayo. Je, una maoni au kisa cha kimaisha tujadili pamoja? Nitumie ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Matukio ya moto yanakwamisha maendeleo, hatua zichukuliwe

HIVI karibuni soko la machinga la Karume liliungua moto na kusababisha mali zao kuteketea, kuacha simanzi na vilio kutokana na hasara kubwa waliyopata watu hao.

Kuungua kwa soko hilo ni mfululizo wa matukio ya moto maeneo mengi nchini ambayo mara nyingi chanzo chake hakijulikani na panapoungua wafanyabiashara hukatazwa kuendelea kupatumia.

Ziko sababu nyingi zinazotolewa kwamba wanatakiwa kupisha uchunguzi wa chanzo cha moto. Pia serikali hutaka kufanya maboresho kwa kujenga miundombinu mipya na bora zaidi.

Uzoefu unaonyesha kuwa baada ya kukamilika kwa miundombinu mipya wafanyabiashara wachache sana humudu kulipa kodi ya vibanda vipya, wengi huanza upya kutafuta pa kufanyia biashara.

Pia uchunguzi na ujenzi huchukua muda mrefu huku maisha ya watu hawa yakiwa yamesimama kwa kuwa mtaji umeteketea na kuanza moja si kazi rahisi.

Nawaza nini huwa ni chanzo cha moto kwenye masoko haya? Nani anahusika? Nini kifanyike kukabili matukio haya ambayo huharibu maisha ya wengi?

Soko hilo limeungua ikiwa bado machungu ya kuungua kwa Soko Kuu la Kariakoo ambalo liliteketea na kusababisha hasara ya mamilioni. Pamoja na kuungua kwa soko hilo, hadi sasa hakuna mfanyabiashara aliyeruhusiwa kurudi kuendelea na shughuli zake huku ikielezwa moto umesababisha harasa kubwa kwa kuwa gharama ya kukarabati jengo hilo ni kubwa sana.

Miongoni mwa wafanyabiashara wako waliokuwa na mikopo kwenye vikoba, SACCOS, taasisi za fedha na benki ambao baadhi masharti yanatambua majanga ya moto, lakini wachache walikata bima kwa ajili ya biashara zao kwamba wanaweza kulipwa na kuendelea na maisha.

Kwa ujumla, ni maumivu na umaskini kwa kuwa maisha yanaanza upya baada ya kilichokuwa tegemeo kupotea na mbaya zaidi hawana namna ya kurudi kuendelea pale walipokuwa.

Maswali mengi kwa jamii hayana majibu hadi sasa kwamba nani anahusika kwenye matukio ya moto,kuna mipango gani mahususi ya kuwasaidia wafanyabiashara kuondokana na majanga au maisha yao kuendelea licha ya kutokea matukio hayo.

Lakini ni muhimu inapojengwa miundombinu mipya ikawatazama wafanyabiashara hao kwamba pamoja na frame za ghali basi kuwe na za bei ya wastani ili nao wamudu na kuendelea na maisha.

Soko la Karume lilitegemewa na wengi wakiwamo wenye maduka sehemu zingine kwenda kufunga mzigo mkubwa hasa wa mitumba na kwenda kuuza. Sehemu hiyo palisifika kwa kuwa na mitumba mizuri daraja la kwanza ambayo wakati mwingine huuzwa bei ya ghali kwenye maduka ya mtaani.

Kadhalika, soko la Kariakoo lilitegemewa sana kwa kuuza pembejeo zote muhimu. Ilikuwa rahisi sana mtu anapotaka pembejeo anazipata kwa kadri ya mahitaji kwenye jengo hilo lakini kwa sasa hazipatikani bali kwenye maeneo yaliyotawanyika.

> **Kwa ujumla, ni maumivu na umaskini kwa kuwa maisha yanaanza upya baada ya kilichokuwa tegemeo kupotea na mbaya zaidi hawana namna ya kurudi kuendelea pale walipokuwa.**

Kwa msingi huo, pamoja na wamiliki kupata hasara,pia wanunuzi nao wamepata usumbufu kwa sababu sasa watazitafuta bidhaa hizo mbali au hawatazipata kwa pamoja eneo moja.

Ni muhimu ripoti za uchunguzi wa masoko haya zikatolewa kwa umma mara baada ya kukamilika na kwa kuwa katika kamati za uchunguzi huwa kuna wataalamu wote waje na mapendekezo ya nini kifanyike kudhibiti hali hiyo na kila mmoja awajibike mwenye eneo lake.

Kwa ujumla, matukio haya yana athiri uchumi wa nchi kwa kuwa watu hawa wamerudi sifuri kimaisha hawana kipato cha kuwawezesha kuendesha maisha kama zamani na kuchangia mzunguko wa fedha na ukuaji wa uchumi.

Ni muhimu kuwa na mikakati ya kukabili matukio hayo ikiwamo kuhamasisha wafanyabiashara kukata bima ya majanga,lakini kuangalia mara kwa mara miundombinu ya umeme ikiwamo kuwatambua wanaojiunganishia kinyemela.

***Mungu ibariki Tanzania***









Ilikuwa siku ya furaha kwa familia ya maharusi Juma Kasim na Nasra Luvanda, baada ya kuamua kufunga ndoa na kuwa mke na mume. Harusi hiyo ilifanyika hivi karibuni na sherehe ya kuwapongeza ilifanyika katika ukumbi wa Jahazi Kisukuru Jijini Dar es Salaam.



# MITINDO

Na Moshi Lusonzo



## VUTIA KIMAHABA

# JEANS, FULANA INATOSHA KUSEMA

VAZI la Jeans awali lilitumika kama nguo za kazi kwa wanaume. Baadaye, lilibadilishwa na kuwa nguo za kawaida kwa wanaume.

Awali jeans ilikuwa ikivaliwa kwa kuambatana na jaketi, sweta na fulana. Mtindo wa denim kwa wanaume umekuwa maarufu na haupitwi na wakati.

Rangi ya bluu mpauko na iliyokolea imekuwa pendwa kwa kila mvaaji wa Jeans. Ni nadra kuona wanaume wakivaa rangi nyekundu au njano.

Jeans ni vazi maalumu pia katika kuvutia wanawake hasa zile zenye kubana na mitindo ya kuchanika maarufu kama 'Craz Jeans'.

Kama unataka kuonekana mtanashati zaidi pale unapotaka kuonana na mpenzi wako kwa mara ya kwanza, basi jeans inayobana kiasi na fulana inatosha kuelezea uhalisia wako.

Kamilisha chini kwa kuvaa viatu kama raba, buti au viatu vya ngozi.

Usisahau kuvaa saa ya kuuweka mkono wako sawa na ikikupendeza zaidi vaa mawani yanayoonyesha macho yako.

## UREMBO

**Na Mary Geofrey**



# VIKUKU
# Pambo la kale linalodumazwa

PAMBO la vikuku limekuwa na mtazamo tofauti katika jamii za Kitanzania, wengi wanalihusisha kama dalili ya uhuni na ukiukaji wa maadili kwa mwanamke.

Lakini kuna baadhi ya makabila, wanatumia pambo hilo kama mila na desturi zao katika kumfanya mwanamke kuwa mrembo zaidi.

Hata hivyo, kwa sasa vikuku huvaliwa kama sehemu ya umaridadi na kuongeza mwonekano wa mtu husika. Hivyo mahitaji yake yamekuwa makubwa.

Pambo hilo linaweza kuwa shanga, ngozi au hata madini kama dhahabu, fedha na shaba.

Kikuku kinaweza kuvaliwa mguu mmoja au miguu yote.

Wanajamii wengi wamekuwa na mtazamo tofauti kuhusu uvaaji wa vikuku wakihusisha na mambo yasiyofaa na kuonyesha kuwa wengi wanaovaa urembo huo wamepotoka au kwenda kinyume na maadili ya kitanzania.

Hata hivyo, wapo baadhi ya watu ambao ni wadau wa urembo wanafafanua kuwa pambo hilo halina maana yoyote livaliwapo kwenye miguu ya mwanamke zaidi ya urembo kama ilivyo kwa hereni na mikufu.

Watu wanashindwa kuelewa kuwa kikuku ni urembo wa mwanamke kama ulivyo urembo mwingine, mfano bangili, hereni, cheni ya shingoni, pete ,vidani na mapambo mengine ambayo hupenda kujiweka mwilini, unajua mwanamke kujipamba

Namna bora ya kukivaa

Kwa mujibu wa wadau wa urembo, kikuku kinapaswa kilegee kidogo katika mguu na kwamba hakipendezi kikiwa kimebana.

Kikibana kinaweza kusababisha matatizo katika kuruhusu damu kutembea, hakiwezi kuwa na mwonekano mzuri kikiwa katika hali hiyo.

Bila shaka katika mitindo inayoonekana kupokelewa vizuri na wanawake hasa wasichana ni pamoja na uvaaji wa vikuku ambao sasa umetikisa katika kila nyanja.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# FURAHIA LADHA
# Juice ya Karoti, Tangawizi, Nanasi



JUICE ni kinywaji kinachoburudisha lakini kinachoongeza vitamini na faida nyingi mwilini.

**Mahitaji**

Nanasi moja kubwa, Tangawizi kiasi zilizosafishwa na kumenywa vizuri na karoti za wastani osha menya katakata vipande vidogo.

**Namna ya kuandaa**

Menya nanasi kisha toa ile sehemu ngumu ya kati kisha kata kata vipande vidogo.

Baada ya kukata kata nanasi vipande vidogo kata karoti na tangawizi na weka katika blenda au juicer.

Saga vizuri ilainike na kisha chuja kwa chujio.

Chukua vipande vya barafu na weka katika bakuli safi ulilochuja ili kuipooza zaidi ili uweze kumpatia mnywaji.

Mchanganyiko huo pia hutumika kama kinga dhidi ya saratani, matumizi ya juisi ya karoti yenye mchanganyiko wa tangawizi husaidia kuukinga mwili dhidi ya matatizo ya saratani za aina mbalimbali.

Juisi hiyo pia husaidia kuua seli zinazoweza kuchangia matatizo ya saratani.

Karoti peke yake kwanza inatosha kwa kuwa mlinzi mzuri wa kinywa, hivyo matumizi ya glasi moja ya juisi ya karoti iliyochanganywa na tangawizi baada ya kula husaidia pia kulinda afya ya kinywa kwa ujumla.

Matumizi ya juisi ya karoti nayo husaidia kuimarisha kinga za mwili na kumlinda mhusika dhidi ya magonjwa mbalimbali yakiwamo matatizo ya macho, kutokana na karoti kuwa na vitamin A ya kutosha.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# MAMBO YA KUZINGATIA KABLA YA KUUZA NYUMBA

BIASHARA ya nyumba na uwekezaji wa majengo ya kisasa inaendelea kushika kasi kila siku.

Lengo la makala hii ni kupeana maarifa kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya kuuza nyumba kwa kujitathmini na kufanya uamuzi sahihi.

Mtaalamu wa masuala ya ujenzi, Christian Kamase, anasema miongoni mwa mambo ya kuzingatia kabla ya kufikia uamuzi wa kuuza nyumba ni kutathmini lengo au sababu kuu ya kufanya hivyo na siyo kukurupuka.

Anasema wakati tulio nao biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo unafanyika kwa mbinu za kisasa ambazo ni matokeo chanya ya ukuaji wa sekta hiyo ya ujenzi inayotokana na mapinduzi ya teknolojia mbalimbali duniani kote.

"Watu binafsi, kampuni na taasisi nyingi zimejitokeza kwa wingi kuzitumia fursa zinazoendelea kujitokeza kila siku kwenye biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo hususani kwa kuiendesha kisasa zaidi kwa kutoa huduma za makazi na biashara kwa wadau mbalimbali," anasema Kamase.

"Lakini kuna baadhi ya watu wamejikuta wakiingia kwenye uuzaji wa majengo au nyumba zao kutokana na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo kwenye maisha ndiyo maana ninashauri kwamba ni muhimu sana ukajitathmini kabla ya kuuza nyumba yako. Jiulize je, unauza nyumba kwa lengo la kibiashara au kutokana na kushindwa kukabiliana na misukosuko ya maisha inayokukabili?

"Kwa mfano hii ni Januari ambayo inajulikana misukosuko yake ya kifedha. Kwa hiyo mtu bila kutulia na kujitathmini unaweza kujikuta unafanya uamuzi wa majuto baadaye," anatahadharisha.

Jambo lingine, anasema endapo kuna ulazima wa kuuza ni vema kabla ya kufanya uamuzi huo, kutathmini bei na gharama ya mauzo ambayo unayapeleka sokoni ili kukusaidia kufahamu kiwango halisi na faida au mapato utakayopata kwa kutimiza malengo unayokusudia.

Mtaalamu huyo anashauri kwamba ni muhimu kuzingatia kwa kuhakikisha nyumba yako inakuwa na muonekano mzuri wa kushawishi wanunuzi, na kwamba kama rangi yake ilikuwa imechakaa ni vyema kuipaka upya pamoja na kuzingatia kuwa inakuwa safi wakati wote.

Anasema mvuto wa nyumba nao utakusaidia kukuongoza pia katika namna ya kufanya tathmini ya bei na itasaidia inunuliwe kwa muda mfupi.

Pia anashauri kwamba kabla ya kufanya uamuzi wa mauzo, ni vema kutathmini hali ya soko la nyumba na si kukurupuka.



## Mapambo yanayobadilisha mwonekano wa madirisha



WATU wengi wanapenda kuwa na nyumba ambayo muonekano wake unakuwa wa kushangaza. Kuna vitu vingi ambavyo unaweza kupamba nyumba na kuifanya iwe ya kipekee katika eneo husika.

Kutokana na umuhimu wake, nakupa dondoo ambazo zitakusaidia kupamba madirisha ya nyumba na kuwa na mwonekano wa kupendeza.


1: Pamba madirisha yako kwa matofali ya kuchoma, hapa unatakiwa kuzungusha madirisha kwa matofali laini ya kuchoma kwani rangi yake itasababisha nyumba kuwa tofauti.

2: Tengeneza kuta za mapambo kuzunguka madirisha ya nyuma. Wengi wanapenda kuweka kuta hizi juu na chini ambazo zinapakwa rangi tofauti na ile ya nyumba.

3: Tengeneza umbo kwenye madirisha yako, njia hii ni nzuri kama ukimpata fundi mzuri wa kutengeneza maumbo kama duara, moyo au kisu.

Jambo la muhimu kabla ya kuweka mapambo ya nyumba, kwanza jaribu kupata ushauri kutoka kwa wataalamu wa ujenzi na mapambo ili kuepuka gharama kubwa za ujenzi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MLA RUSHWA 'ORIJINO ILIYOMKOLEA' HAWEZI KUROPOKA KAMA WEWE ETI NIKUKAMATE UMESHAKULA RUSHWA! WEWE NI MLEVI TU.
HAYA CHELEWA CHELEWA NIKAMATWE NA WENGINE
SEMA RISHIDA RAKO NIKUHUDUMIE USINIREGESEE MIMACHO
NAOMBA KUJUA HUDUMA ZENU PLIZI
USIJIZIME DATA ACHA MAKELELE UJAVAA KINGA
KWENDA ZAKO HUKO! NATAMBA NIMECHANJA WEWE UNATAMBIA NINI?
HUYO ANAYESEMA AMECHANJA NAMJUA VIZURI SANA...AKAE KWA KUTULIA HUMU
WENGI HUMU MNACHANJA MBUGA!
ACHENI MZAHA 'UJANJA KUCHANJA' TUSIZINGUANE
TOKA BASI TUKATEKELEZE MAJUKUMU YETU
WEWE NAWE KILA SIKU KUJIGEUZA NYAU UCHOKI? JANA NIMEKUNG'UTWA JIWE LA KICHWA NUSU NIFE!
PESA NILIZOCHANGIA KADI HIZI NIKIPIGA 'KALUKULESHENI' NITAZIKWA!
UNAONA JE 'NTATOBOA?'
KWA SINDANO AU SPOKU?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...FUMBA MACHO USIONE JAPO UNAONA

# Waliokufa shambulio la Yemen wafikia 80

**SANAA,** YEMEN

WAKATI muungano wa kijeshi unaoongozwa na Saudia ukikanusha kuhusika na shambulio la anga lililolenga gereza lililo chini ya waasi wa Houthi nchini Yemen, idadi ya waliokufa kwenye mashambulizi hayo ni zaidi ya watu 80.

Ofisi ya Habari ya waasi wa Houthi iliripoti idadi hiyo ya vifo ikiendelea kusema kuwa, bado waokoaji wanaendelea kuwatafuta majeruhi na mabaki ya miili ya watu wengine wanaohofiwa kufa kwenye eneo la gereza hilo Kaskazini mwa Saada mpakani na Saudi Arabia.

Tukio hilo la Ijumaa ni sehemu ya mashambulizi ya angani na ardhini yanayozidi kuchochea mzozo wa Yemen yenye vita ya wenyewe kwa wenyewe iliyodumu kwa miaka kadhaa.

Katika hatua nyingine, Shirika la Habari la SPA la Saudia limeripoti kuwa, muungano wa kijeshi unaoongozwa na Saudia kupitia kwa msemaji wake lililotoa ripoti kwamba walishambulia gereza hilo sio za kweli na kwamba wataijulisha ofisi ya masuala ya haki za binadamu ya Yemen pamoja na kamati ya kimataifa ya msalaba mwekundu kuhusu ukweli na taarifa zaidi.

Shambulio hilo limeibua ukosoaji wa muungano wa kijeshi unaoongozwa na Saudia kutoka kwa Umoja wa Mataifa, Mashirika ya misaada ya kimataifa na makundi ya kutetea haki za binadamu.

Kwa mujibu wa shirika la hisani la madaktari wasio na mipaka, karibu watu 200, walijeruhiwa katika shambulio hilo la anga lililofanywa jana Ijumaa.

Wakati waasi wakidaiwa kutumia udanganyifu kwenye mzozo

Msemaji wa muungano huo wa kijeshi Brigedia Jenerali Turki al-Malki, aliwatuhumu waasi wa Houthi kuwa, hawakutoa taarifa kwa kamati ya kimataifa ya msalaba mwekundu kuwa eneo la gereza lililolipuliwa ni moja ya sehemu zinazohitaji ulinzi dhidi ya mashambulizi ya anga.

Alidai kuwa, kushindwa kwa waasi hao kufanya hivyo kuna akisi kawaida ya wapiganaji hao ya kutumia njia za udanganyifu katika mzozo huo.

Waasi wa Houthi walikuwa wakitumia gereza lililoshambuliwa kuwashikilia wahamiaji waliokamatwa wengi wao wakiwa ni Waafrika waliokuwa wakijaribu kuelekea Saudi Arabia kupitia Yemen.

Mzozo katika taifa hilo masikini la kiarabu ulianza mwaka 2014 wakati waasi wa Houthi walipoudhibiti mji mkuu Sanaa na sehemu kubwa ya kaskazini mwa Yemen na hivyo kuilazimu serikali kukimbilia kusini na kisha uhamishoni nchini Saudi Arabia.

Muungano wa kijeshi unaoongozwa na Saudia, wakati huo ukiungwa mkono na Marekani, uliingia vitani miezi kadhaa baadae katika jaribio la kuirejesha serikali madarakani.

Mgogoro huo ulikuwa moja kati ya mizozo mibaya zaidi ya kiutu duniani huku jumuiya ya kimataifa ikikosoa mashambulizi ya anga ya Saudia ambayo yamewauwa mamia ya raia na kuharibu miundo mbinu ya serikali.

Waasi wa Houthi kwa upande wao walikuwa wakiwatumia watoto kama sehemu ya wapiganaji wao na kuweka mabomu ya ardhini kote nchini humo

**DW**

# Watu 6 wafariki kwa moto

**NEW DELH,** INDIA

WATU wasiopungua sita wamekufa na wengine 25 wamejeruhiwa baada ya moto mkubwa kuzuka kwenye jengo la ghorofa 20 katika mji wa kibiashara wa Mumbai nchini India.

Duru zinasema watu wanne miongoni mwa waliojeruhiwa, wako kwenye hali mahututi huku wazee sita waliookolewa wakipelekwa kwenye hospitali ya karibu kupatiwa huduma ya hewa ya Oksijeni.

Mikanda ya video iliyorushwa kupitia televisheni imeonyesha wingu zito la moshi likiwa limetanda angani lakini maofisa wa serikali walisema moto tayari umedhibitiwa baada ya juhudi za karibu saa tatu.

Meya wa Mji huo Kishori Pednekar, alisema chanzo cha moto huo huenda ni hitilafu ya umeme na uchunguzi umeanzishwa kubaini sababu halisi ya mkasa huo.

Mifumo mikongwe ya umeme imekuwa chanzo cha ajali za moto za kila wakati nchini India na madhara huwa makubwa kutokana na kanuni dhaifu za usalama na kukosekana njia za watu kujiokoa.

**DW**



Polisi wakiwa wanalinda jengo la Kamla mjini Mumbai nchini India baada ya kuibuka kwa moto katika ghorofa ya 19 na kusababisha vifo vya watu sita jana **(PICHA: PTI)**

# UN yaitaka Taliban itoe taarifa

**KABUL,** AFGHANISTAN

UMOJA wa Mataifa jana umelitolea wito kundi la Taliban, linaloongoza Afghanistan kutoa taarifa za waliko wanaharakati wawili wa haki za wanawake ambao wanadaiwa kuchukuliwa kwa nguvu kutoka majumbani mwao mjini Kabul siku kadhaa zilizopita.

Katika taarifa yake kupitia ukurasa wa Twitter, ujumbe wa Umoja wa Mataifa nchini, Afghanistan ulielezea wasiwasi mkubwa kuhusiana na kutoweka kwa Tamana Paryani and Parwana Ibrahimkhel wanaofahamika kuwa wapinzani wakubwa wa utawala wa Taliban.

Baada ya kutoweka kwao siku ya Jumatano usiku, mkanda wa video uliorekodiwa na Paryani ulisambaa kwenye mitandao ya kijamii ukionyesha mwanaharakati huyo akiomba msaada wakati wanaume waonadaiwa kuwa maafisa wa kundi la Taliban wakigonga mlango wa nyumbani kwake. Mamlaka nchini Afghanistan zimekanusha kuwashikilia wanaharakati hao waliokuwa wakiongoza kampeni ya kupinga sera za Taliban zinazowazuia wanawake kusoma au kufanya kazi.

**DW**

# Sudan kusaka suluhu na Ethiopia

**KHARTOUM,** SUDAN

KIONGOZI mwandamizi wa Sudan, Mohamed Hamdan Dagalo, ameelekea Ethiopia, kwa ziara ya nadra ya Ofisa wa Serikali tangu mataifa hayo mawili yalipotumbukia kwenye mivutano kuhusu mipaka.

Shirika la Habari la Sudan (SUNA), limeripoti kuwa Daglo, ambaye ni kiongozi wa pili wa ngazi ya juu katika baraza la utawala la kijeshi nchini Sudan, atakuwa Ethiopia kwa siku mbili ili kukutana na maofisa kadhaa wa nchi hiyo.

Ofisa huyo ni Mkuu wa kikosi maalumu chenye nguvu cha RDF, kinachoogopwa kutokana na rekodi yake ya vitendo vya ukatili hasa katika jimbo la magharibi la Darfur.

Mahusiano kati ya Sudan na Ethiopia yamezorota kutokana na mzozo juu ya eneo la mpaka linalozozaniwa la Al-Fashaqa Magharibi ambalo kila upande linadai haki ya umiliki.

**DW**

# Visiwa vya Kiribati, Samoa vyapambana na COVID-19

**CANBERRA,** AUSTRALIA

VISIWA viwili vidogo vya Bahari ya Pasifiki vya Kiribati na Samoa, vimetangaza kufunga shughuli zote za kawaida jana, baada ya kubainika visa kadhaa vya virusi vya corona kutoka kwa wasafiri wa kigeni waliowasili siku za hivi karibuni.

Serikali ya Kiribati ilisema hatua hiyo inafuatia kuthibitika kwa visa kadhaa vya maambukizi ya COVID-19 miongoni mwa wasafiri waliowasili kutoka kisiwa jirani cha Fiji pamoja na kisa kingine kilichobanika kwenye Mji Mkuu wa taifa hilo katika kisiwa cha Samoa.

Waziri Mkuu, Fiame Naomi Mata'afa, alisema uamuzi huo umefikiwa baada ya kuongozeka kwa visa vya COVID-19 kutoka kundi la abiria waliowasili kutoka Australia.

Tangu kuzuka kwa janga la corona visiwa hivyo viwili vimefanikiwa kuepuka idadi kubwa ya maambukizi ya COVID-19.

Hadi mwezi uliopita, Kiribati haikuwa na kisa hata kimoja cha maradhi hayo huku kisiwa cha Samoa kilirikodi visa viwili pekee tangu kuanza kwa janga hilo.

**DW**

## MAKALA

# RAI YANGU KWA LATRA JUU YA SEATING BELT



Na Magabilo Masambu

**Hatari ya mikanda ambayo inatumika sasa, ambayo inafunga kiuno pekee haimsaidii abiria kujizuia kurudi nyuma au kwenda mbele, kitu ambacho kinapingana na sheria ya kwanza ya Newton (1st Newton's law of motion).**

BADO niko katika mwendelezo wa makala juu ya kuangazia usalama wa abiria katika vyombo vya moto. Juma lililopita nilizungumzia juu ya mwendokasi wa vyombo vya moto hasa magari ya baadhi ya viongozi wa serikali kutojali na kutii sheria na alama za barabarani kwa kisingizio cha kuwahi mikutano na vikao, jambo ambalo ama linaweza kugharimu maisha yao au ya wale wanaoongozana nao katika misafara.

Juma hili natoa rai yangu kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kuhusu mikanda (Seating belt) wanayopaswa kuvaa au kuifunga abiria kwa ajili ya usalama wao wawapo safarini.

Dhana ya kufunga mikanda katika magari inatokana na sheria ya mwanasayansi wa zamani, Isack Newton. Hii ni kati ya sheria tatu ambazo zinazungumzia mwendo wa vitu mbalimbali kama magari, pikipiki na risasi katika bunduki.

Sheria ya kwanza inayoitwa "First Newton's law of motion" inazungumzia kitendo cha kitu kutokubaliana na ukweli yaani "The law of inertia". Nikizungumzia katika muktadha wa usafiri wa vyombo vya moto, mfano gari, huwa inatokea kwamba ikiwa abiria wamesimama ndani ya gari dereva ghafla akaondoa gari, basi abiria wote wataangukia kisogo kwa maana ya kurudi nyuma na ikiwa gari liko kwenye mwendo ghafla dereva akafunga breki basi huwa abiria wanaangukia paji la uso kwa maana ya kuelekea mbele.

Maana yangu ni kwamba mikanda inayotumika kwenye mabasi ya abiria karibu yote haifai kutumika kulinda usalama wa abiria, pengine naweza kusema kwamba, mikanda hiyo ni hatari zaidi pale inapotokea ajali. Sababu yake ni kwamba mikanda ya usalama inapaswa kudhibiti mjongeo (movement) wa abiria katika maeneo makuu mawili. Moja ni kudhibiti mjongeo wa abiria kuelekea juu (upward motion) kudundadunda, pili mkanda huo unatakiwa kuthibiti mjongeo wa abiria kurudi nyuma pale gari linapokwenda mbele au pale gari linaposimama ghafla.

Hatari ya mikanda ambayo inatumika sasa, ambayo inafunga kiuno pekee haimsaidii abiria kujizuia kurudi nyuma au kwenda mbele, kitu ambacho kinapingana na sheria ya kwanza ya Newton (1st Newton's law of motion). Ikitokea ajali wakati abiria amefunga kiuno pekee, kuna uwezekano wa kukatwa kiuno au kumzuia kujinasua kwani atakuwa amefunga kiuno huku kiwiliwili chote kikijipigiza huku na kule mwishowe anakufa kwa kujibamiza akiwa kwenye kitanzi.

Kazi pekee ya mikanda ya kiuno wanayofunga abiria ni kuzuia abiria kujirusha juu (upward motion) kitu ambacho kwa sasa kutokana na barabara kuwa za lami hakipo, labda mara chache kwa abiria wanaokaa viti vya nyuma pale gari linapokuwa linapita kwenye matuta. Mikanda kama hiyo ilifaa sana wakati barabara ni za vumbi na mashimo kibao.

Mara kadhaa nimewahi kubishana na askari wa usalama barabarani kuhusu kutovaa mkanda kwa sababu siwezi kukubali kuvaa kitanzi ambacho najua likitokea la kutokea hakitanisaidia chochote zaidi kitasababisha nisijinasue. Sina hakika kama jambo hili huwa linanikera peke yangu.

Ni kweli kwamba makondakta wanafanya kazi yao ya kutangaza kuvaa mikanda, lakini binafsi huwa sioni kama mkanda huo unaweza kunisaidia chochote katika kuokoa maisha yangu ikiwa ajali imetokea.

Kinachotakiwa kufanyika ni kwamba kama yalivyo magari ya binafsi ambapo kuna mikanda ya aina mbili yaani mmoja unafunga kiuno ili usiruke juu na mkanda mwingine unafunga kifua ili usiende mbele ama nyuma hapo abiria anakuwa salama maana yake ni kwamba. Hata likitokea gari likapata ajali, asilimia kubwa ya abiria watasalia kwenye viti vyao hata gari libingilike mara 10.

Abiria watakuwa pale pale na hawataumia kwa kujigonga kwenye machuma labda itokee viti ving'oke.

Najaribu kufikiri inakuwaje magari ya binafsi yawe na mikanda miwili ya usalama ilhali yanayobeba mamia ya abiria yana mkanda unaofunga kiuno pekee? Mikanda ya kufunga viuno vyetu, tayari tunayo kwenye suaruali zetu tunahitaji mikanda ya usalama wa maisha yetu.

Ushauri wangu kwa LATRA, mkiwa ndiyo wenye mamlaka ya kudhibiti usafiri wa nchi kavu ni muhimu kuona uwezekano wa kuyafanya mabasi yote Tanzania kuwa na mikanda ya usalama badala ya vitanzi vilivyomo sasa. Kama mabasi yanakuja na mkanda mmoja wa kiuno basi iwe juu ya mmiliki wa basi kuhakikisha mikanda ya kifuani inawekwa. Kwa kufanya hivyo, abiria watasafiri kwa raha huku usalama wao ukiwa mkubwa zaidi. Wahenga wanasema kinga ni bora kuliko tiba.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Mambo kwa Soksi ulivyokataliwa RTD



Na Adam Fungamwango

**'Mambo Kwa Soksi'. Ni wimbo uliopigwa na Super Matimila iliyokuwa chini ya Dk. Remmy Ongalla. Ulikuwa unahimiza utumiaji wa mipira ya kiume, hasa wakati ule miaka ya 1980 ndiyo kwanza Ukimwi ulikuwa unaingia nchini na wengi hawakuwa na elimu hiyo.**

MIAKA ya hivi karibuni tumeshuhudia nyimbo nyingi hasa za muziki wa kizazi kipya zikiwa na maneno yenye ukakasi mkubwa. Nyimbo zimekuwa na maneno ambayo si mafumbo wala nahau, badala yake yamekuwa maneno yanayotafsirika moja kwa moja hata kwa watoto wadogo.

Mbaya zaidi si maneno mazuri kwenye jamii. Baadhi ya wasanii wa kizazi kipya wanaona kuwa kuimba maneno yenya utata ndiyo wimbo utapendwa au kupokewa vizuri na mashabiki. Na nadhani hata mashabiki wa muziki wa sasa baadhi yao wamekuwa mashabiki na maneno haya.

Zamani ili wimbo ukubalike kurekodiwa ni lazima uweke maneno ambayo hayatotafsirika moja kwa moja kwa jamii. Ni lazima wale wenye kutazama kwa jicho la tatu, washairi na malenga ndio wanaoweza kujua nini kinaimbwa na tafsiri yake ni nini.

Mfano kuna wimbo mmoja wa taarabu 'Bunduki Bila Risasi Yaua Namna Gani?', ulioimbwa na marehemu Bi, Shakira Said. Ni aghalabu sana kugundua nini alichokuwa akikikusudia tofauti na baadhi ya wasanii wa sasa ambao wamekuwa wakiweka wazi sana.

Kuna baadhi ya nyimbo za bendi mbalimbali ambazo hadi leo hii hazijarekodiwa hadi bendi hizo zimekufa, zingine zilirekebishwa maneno wakati wa kurekodi na zingine zilipigwa marufuku baada ya kurekodiwa.

Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD), wakati huo ambayo kwa sasa ni TBC Taifa, ilikuwa na kamati iliyokuwa inapitia maneno ya nyimbo zote ambazo zililetwa kurekodiwa. Kabla ya kurekodi, bendi zililazimika kuleta mashairi ya nyimbo zote na kamati inayapitia neno ya neno.

Huko ndiko baadhi ya maneno yanakatwa na kuambiwa watumie maneno ambayo kamati imependekeza au ambayo wanamuziki wenyewe wataona inafaa. Baada ya kurekebishwa bendi inakwenda kurekodi.

Si hivyo tu, inawezekana wimbo ukarekodiwa, lakini baada ya kutoka wananchi wakaupokea vinginevyo tofauti na ilivyotarajiwa, basi unaweza pia ukazuiwa kupigwa redioni.

Lengo la kamati kuzipitia, kuzirekebisha, kuzikataa na hata kuzipiga marufuku baadhi ya nyimbo ni kutoifanya jamii ya Watanzania kupotoka, kutoka kwenye utamaduni wao halisi na kuiga wa wengine, kuheshimiana, kuwa na adabu na heshima, yaani mkubwa na mdogo kuheshimiana, kusimamia maadili ya kitaifa lakini pia kuwafanya kuwa wamoja, wenye amani, utulivu na mshikamano.

Tutaanza kuzipitia zote zilizorekodiwa lakini zikapigwa marufuku baadaye, zilizorekebishwa maneno ambapo awali zilikuwa na maneno mengine, ila leo tuanze na nyimbo ambazo zilitungwa na bendi mbalimbali na hazijawahi kurekodiwa kwa sababu mbalimbali ambazo nimeziainisha na zingine zinazofanana na hizo.

Baada ya kukataliwa zikabaki kupigwa kwenye kumbi tu, za zilikuwa zinapendwa na mashabiki wengi.

'Mambo Kwa Soksi'. Ni wimbo uliopigwa na Super Matimila iliyokuwa chini ya Dk. Remmy Ongalla. Ulikuwa unahimiza utumiaji wa mipira ya kiume, hasa wakati ule miaka ya 1980 ndiyo kwanza Ukimwi ulikuwa unaingia nchini na wengi hawakuwa na elimu hiyo.

Kwa bahati mbaya sana bado nchi ilikuwa na usiri kuhusu mambo hayo, tofauti na sasa ugonjwa huo na hata jinsi ya kujikinga unazungumziwa kwa uwazi mkubwa, kiasi kwamba kuna matangazo kwenye redio na televisheni, vipeperushi na hata mabango. Wimbo ukapigwa marufuku.

Ungerekodiwa sasa nadhani ungepewa tuzo na wizara husika ya mambo ya afya.

Remmy alikuwa mjanja tangu zamani, wimbo huo akaenda kurekodi nchini Kenya, hivyo watu walikuwa na kanda zao mitaani wakiusikiliza, lakini huwezi kuusikia kwenye redio.

Nyimbo nyingine ni 'Kanyaboya', 'Cha Mlevi Huliwa na Mgema', na 'Dalila' zote za Juwata Jazz, Msondo Ngoma kutokana na sababu nilizoeleza hapo juu kuhusu maadili ya jamii.

Orchestra Safari Sound 'Ndekule' wao walikataliwa kurekodi nyimbo za 'Jabali', ulioimbwa kwa kiasi kikubwa na Muhidini Gurumo, na 'Nyama ya Nyani' uliotungwa na Molay Tunga ambaye baadaye mashabiki walimpachika jina la Nyama ya Nyani kutokana na wimbo huo ambao pamoja na kukataliwa kurekodiwa RTD, ulipendwa mno ukumbini.

Wiki ijayo tutaziangalia nyimbo ambazo awali zilikuwa na maneno fulani, ambayo yalirekebishwa kabla ya kurekodiwa kwa amri ya kamati ya RTD.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

# Ajenda ya siri-14

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ILIBIDI Eddy abadilishe hadithi na kujitambulisha kuwa hajafika pale kufuata mashamba, ila ni askari polisi aliyekuja kumuuliza maswali kadhaa yanayohusu maisha ya marehemu Hafidh Chilambo, ikiwamo siku ya tukio ambapo aliuawa. Eddy alitoa kitambulisho cha uongo.

"Ni kwamba Tina amehukumiwa kunyongwa, lakini kuna watu bado wanatafutwa wafunguliwe mashtaka. Wewe ulikuwa mlinzi kwenye nyumba hiyo. Na taarifa nilizozipata kuwa uliacha au kuachishwa kazi wiki moja baada ya tukio hilo. Sina ugomvi na wewe mzee, na wala serikali haina matatizo na wewe. Jibu ambalo nitakalokuuliza na ambalo unalifahamu tu basi. La sivyo na wewe utafunguliwa mashtaka."

Mshangao na woga mkubwa ulimpata mzee Kalango. Alionekana kutetemeka. "Usiogope mzee, sema tu unayoyajua na kujibu maswali yangu kwa ufasaha, basi."

"Sawa kijana nitajibu yote." Alijibu kwa hofu.


Mwahija ndiye aliyeifanya kazi ya kumfahamisha na kumuelekeza mzee Kalango anakoishi. Eddy, pamoja na mapenzi, alianza kumtumia msichana huyo kwenye mambo yake ya kipelelezi bila yeye kujijua.

Alichoambiwa kukifanya ni kujua mlinzi wa zamani kwenye nyumba hiyo yuko wapi. Aliambiwa kuwa huyo ndiye anayejua Tina alifanya kazi miaka mingapi na akimpata hawezi kumuongopea, tofauti na mke wa marehemu na ndugu wengine. Mwahija alidanganywa na Eddy kuwa anachotaka kupata stahiki zote za Tina, ili akampoze mama yake kijijini na yeye akakubali kuifanya kazi hiyo bila kujua.

Alishindwa kujiuliza mtu ambaye ameshaua na kuhukumiwa, anapataje tena haki ya kulipwa?

Kifupi ni kwamba alikuwa amedanganywa na mpelelezi Eddy ambaye mpaka sasa alikuwa hajamfahamu ni nani zaidi ya mpenzi wake na akadanganyika. Akaifanya kazi hiyo vizuri tu.

Mfamasia huyo ambaye ofisi yake ya duka la madawa haipo mbali sana na nyumba hiyo, aliteta na kuongea na majirani, hatimaye mmoja akamwambia kuwa anaitwa mzee Kalango, alikutana naye Goba. Na akamuelekeza sehemu anayoishi. Eddy alipewa taarifa na ramani na mpenzi wake, hiyo ndiyo aliyotumia kufika pale.




**Ni kutotaka kutotambulika kama yeye ni nani. Hivyo anaweza kutambulika au kujitambulisha kama mwandishi wa habari, askari polisi, mwanamuziki, muuza magazeti, dereva, meneja wa baa, au kazi yoyote ile kulingana na kile ambacho anahitaji kukipata na katika mazingira husika.**

"Una uhakika na haya unayoyasema?"

"Yaani afande haya ninayoyasema ni kweli kabisa."

"Huyu hausiboi yeye anaishi wapi?"

"Mbagala transifoma, wenyewe wanapaita Foma, ukifika Mbagala Kuu, unapanda mabasi ya kwenda Chamazi au Chanika, mbele kama kituo cha pili au cha tatu, kuna kituo kinaitwa transifoma, unashuka pale pale, unaingia kulia kwenye barabara ya mchanga, nyumba ya kwanza ya pili, ya tatu ndiyo hiyo hiyo."

Kidogo Eddy aangue kicheko, kwani uelekezaji wa mzee Kalango ulionyesha kabisa kuwa kama akitaka kwenda, apande daladala tu, na hamuelekezi kama mtu ambaye anakwenda na gari yake.

Hata hivyo, haikuathiri chochote. Alimuaga mzee huyo ambaye alikuwa kwa mbali anatetemeka kutokana na maswali aliyokuwa akiulizwa, huku akipigwa mkwara kuwa kama hatojibu kwa usahihi basi baadaye anaweza kupelekwa na yeye mahakamani kwa ajili ya kesi hiyo, kwani haijaisha na kuna wahusika wengi wanatafutwa kwa kesi hiyo."

Moja kati ya vitu vingi ambavyo anatakiwa kuwa navyo mpelelezi ni sanaa ya uongo. Sanaa ya hadaa au kudanganya. Mpelelezi aliyeiva anakuwa na sanaa ya uongo kwa kiwango cha hali ya juu na huwa wanafundishwa hivyo.

Unatumika kwa ajili kuficha utambulisho wake, badala yake atakuwa na vitambulisho mbalimbali vya bandia, hata pasipoti. Ni kutotaka kutotambulika kama yeye ni nani. Hivyo anaweza kutambulika au kujitambulisha kama mwandishi wa habari, askari polisi, mwanamuziki, muuza magazeti, dereva, meneja wa baa, au kazi yoyote ile kulingana na kile ambacho anahitaji kukipata na katika mazingira husika.

Lengo ni kutaka kufika anapopahitaji, au jinsi ya kupata habari fulani anayoihitaji. Ni kwa sababu habari za kipelelezi hutafutwa kwa kujifanya ni mtu fulani, kumpa mtu taarifa feki ili akupe taarifa kamili, au kumpa sifa za uongo. Ni mbinu kubwa inayotumika. Kimsingi ni waongo waliofundishwa sanaa ya uongo, lakini ni uongo wenye faida kwa jamii na taifa kwa jumla.

Ndiyo maana alijifanya askari polisi, ili kumtisha mzee wa watu kiasi cha kuongea anachokielewa bila kuficha, au kuongopa, lakini pia akiongezea kumtisha kuwa kuna watu bado wanasakwa wakaunganishwe, hivyo kuongea ukweli ndiyo kutawafanya wao kama askari kujua kama huenda alihusika au la. Kifupi ni kwamba Eddy alijua mzee huyo hahusiki na lolote, ila alijua huenda ni mtu anayefahamu angalau mambo mawili matatu ya ndani ya nyumba ya Fadhili Chilambo ambayo yangeweza kumsaidia.

Uongo huo huo, ulimsaidia kumfanya kumpa kazi mpenzi wake Mwahija bila kujijua kutafuta anakoishi mzee Kalango.

Alichomoa noti mbili za shilingi elfu ishirini, akamkabidhi noti moja ya shilingi elfu kumi mzee Kalango.

Hakuamini alichokiona. Mtu ambaye alikuwa akimuuliza maswali ya kipolisi, huku akimtahadharisha kuwa kitamkuta kitu kibaya kama akiwa anaongopa kwenye majibu yake. Sasa anampa pesa. Ni kitu ambacho hakutegemea.

"Mzee utakwenda kupata japo kahawa. Samahani sana kwa usumbufu." Ni maneno ambayo hakutarajia kuyasikia masikioni kwake kutoka kwa askari ambaye alimfuata kikazi.

"Au amefurahi nimemjibu maswali yake vizuri?" Alijiuliza na hapo hapo alijikuta akijibu "Ahsante sana, ahsante Mungu akubariki."

Eddy hakujibu kitu, badala yake akamtuma amuitie mkewe.

"Alisogea hatua kadhaa, na kumwita "We mama Bupe, unaitwa huku."

Alikuwa ndani akiwa anatega sikio. Ujio wa mgeni huyo ulimtisha sana mama huyo, hivyo alisikia kila kitu kilichokuwa kikiongelewa. Maswali na majibu yote yaliingia masikioni mwake.

Wito ule ulimshtua zaidi ya kile kilichomshtua mwanzo. Aliitikia, lakini sauti haikutoka kwa woga.

Alijikuta akitoka nje, akiwa anajivuta kama mbuzi anayekwenda machinjioni.

"Huyu ndiye aliyenikaribisha. Ahasante sana mama, nitakuja siku nyingine." Alisema naye akimfuata na kumpa noti iliyobaki mkononi mwake ya shilingi elfu kumi.

Woga na mshangao alioupata mama Bupe alishindwa hata kuipokea pesa hiyo, na badala yake mikono yake ilishindwa kufanya kazi kutokana na ganzi, ikaanguka chini na kuanza kupeperuka na upepo. Haraka mzee Kalango alifanikiwa kuiokota.

"Nipe hela yangu." Mama Bupe alimwambia mumewe.


"Unapokea pesa kizembezembe, nitaichukua mimi na hii."

Eddy aliangua kicheko dhaifu na kusema "Hapana mzee mpe mama, alikosea tu kuipokea."

Mzee Kalango kidogo imani ilimrudia. Aliona askari huyo hakuja kwa nia mbaya. Na kwa bahati nzuri na yeye aliamua kuongea kila kitu ukweli kama ulivyo.

**ITAENDELEA JUMAPILI**

## HABARI BURUDANI



# BILA BILIONI 1.6 HUMPATI ADELE

UKISIKIA kiasi ambacho hulipwa mwanamuziki wa Uingereza, Adele, utabaki ukijiuma midomo! Unaambiwa shoo yake moja tu anayotakiwa kuburudisha huingiza mfukoni mwake dola 700,000, sawa na shilingi bilioni 1.6.

Taarifa hizo zimeibuka baada ya kulipwa kiasi hicho katika onyesho moja lililofanyika huko Las Vegas Nevada Marekani.

Inaelezwa sio ukilipa pesa hizo utakuwa umemaliza kila kitu, bali utaambatanisha na chumba atakacholala chenye thamani ya dola 30,000 ambazo ni sawa na milioni 70 za kitanzania.

Adele kwasasa anapeta na album yake mpya aliyoingiza Sokoni mwaka jana inayokwenda kwa jina la 30.

# NEY

## WA MITEGO ACHA KUWATISHA

SASA imekuwa tabu! Ndivyo rapa mkali hapa nchini Ney wa Mitego, anavyotamba na kujifananisha na kioo ambacho kila akitembea anaiona sura yake pekee.

Ney wa Mitego ambaye anatambulika kama 'The Trueboy' amesema siku hizi hakuna ushindani katika muziki huo kiasi ambacho amekuwa na hamu ya kuwa na msanii anayeshindana naye.

"Wasanii wengine wa rap wapo wapi kwani mbona siwaoni, najiona mimi tu kila kona mtaani mpaka kwenye trending zao nipo mimi tu na hunijui, namiss ule ushindani kweli" ameandika Ney wa Mitego



# Vanessa utarudi tu kwenye muziki

SASA ni wazi Vanessa Mdee, ambaye ametangaza kuacha muziki atalazimika kurudi kwa muda baada ya jina lake kutajwa kuwania tuzo za muziki ya Uingereza zinazojulikana kama Urban Music Awards.

Katika tuzo hizo Vanessa anagombania kipengele cha Mwanzamuziki wa mwaka kutoka Afrika pamoja na msanii mwingine kutoka Tanzania Naseeb Abdul maarufu kama Diamond.

Aidha, kipengele hicho kinawaniwa pia na wasanii wengine kutoka nchi mbalimbali,ambao ni Tiwasavage, Wizkid,Olakira, Davido,Burna Boy, Falz, Joe Boy na Rema.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAALAND HAITAKI MAN

KLABU ya Manchester United imefutilia mbali mpango wa kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland baada ya kufahamishwa kuwa kiungo huyo wa kimataifa wa Norway mwenye umri wa miaka 21 angependa kuhamia Real Madrid. ***(ESPN)***

### STERLING NA BARCA

NYOTA wa England, Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 27 alikuwa tayari kujiunga na Barcelona kwa mkopo kutoka Manchester City kabla ya klabu hiyo ya LaLiga kuamua kumsajili winga wa Hispania, Ferran Torres mwenye umri wa miaka 21. ***(Athletic )***

### VLAHOVIC AITAMAINI EPL

MSHAMBULIAJI wa Fiorentina, Dusan Vlahovic ana "ndoto" ya kucheza kwenye Ligi Kuu England, lakini kiungo huyo wa kimataifa wa Serbia mwenye umri wa miaka 21-anataka kujiunga na Manchester City badala ya Arsenal. ***(La Repubblica)***

### MCGINN AWANIWA MAN

KLABU ya Manchester United inamnyatia kiungo wa kati wa Aston Villa na Scotland, John McGinn mwenye umri wa miaka 27 katika uhamisho wa msimu wa joto. ***(Telegraph)***

### BARISIC ATAKIWA

MLINZI wa Rangers, Borna Barisic mwenye umri wa miaka 29, amethibitisha kuwa kuna klabu iliyowasilisha ombi la kumnunua awali katika dirisha la uhamisho, licha ya tetesi zinazomhusisha kiungo huyo wa kimataifa wa Croatia, Watford na Aston Villa. ***(Sky Sports)***

### MELO HAKIELEWEKI

MAZUNGUMZO ya Arsenal na Juventus kuhusu mkataba wa mkopo wa kiungo, Arthur Melo yamekwama kwa sababu klabu hiyo ya Serie A bado haijapata mbadala wa Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 25. ***(Tuttomercatoweb, via Express)***

### TCHOUAMENI KUTUA CHELSEA

CHELSEA huenda ikapewa nafasi ya kumsajili kiungo wa kati wa Monaco, Mfaransa Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 21, huku Manchester United wakielekeza darubini yao kwa kiungo wa RB Leipzig na Mali, Amadou Haidara mwenye umri wa miaka 23, na kiungo wa Borussia Monchengladbach na Uswisi mwenye umri wa miaka 25, Denis Zakaria. ***(Football.london)***

### COSTA AITAKA CORINTHIANS

DIEGO Costa mwenye umri wa miaka 33 ambaye anahusishwa na Arsenal anataka kuhamia klabu ya Brazil ya Corinthians, ambako huenda akaungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Chelsea, William. ***(Evening Standard)***

### MILINKOVIC-SAVIC HUYO MAN

MANCHESTER United ipo mbele ya Juventus na Inter Milan katika mbio za kumsaka kiungo wa kati wa Serbia, Sergej Milinkovic-Savic mwenye umri wa miaka 26 kutoka Lazio. ***(Il Messaggero via Sport Witness)***

### HAZARD SASA KUONDOKA

MSHAMBULIAJI wa Ubelgiji, Eden Hazard anataka kuondoka Real Madrid, lakini hana mpango wa kujiunga na Newcastle, ambao walikuwa wamewasilisha dau la pauni milioni 41.3 kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31. ***(El Nacional)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL: CHELSEA ITASAJILI JANUARI HII

**Asema wanakabiliwa na majeruhi hivyo itawalazimu kuingia sokoni kuimarisha kikosi...**

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel hajaondoa uwezekano wa kufanya usajili katika dirisha hili dogo la Januari.

Blues hao wamejikuta kwenye wakati mgumu wa kuwania taji la Ligi Kuu baada ya kupoteza kwenye mechi zake hivi karibuni, ikiwa haijashinda mechi nne za Ligi Kuu walizocheza ugenini na imeshinda mara mbili tu kati ya mechi tisa zilizopita.

Kwa sasa wamepitwa pointi 12 na vinara wa Ligi hiyo, Manchester City wakiwa wamecheza mchezo mmoja zaidi.

Alipoulizwa kuelekea mchezo wa leo Jumapili dhidi ya Tottenham kama kutakuwa na ongezeko la wachezaji Januari hii, Tuchel alijibu: "Siwezi kusema hapana. Pia sishawishiki kwamba kila kitu kitakuwa sawa. Ngoja tusubiri tuone."

Mchezo dhidi ya Spurs wa pale Stamford Bridge utakuwa ni wa 16 kwa Chelsea tangu Desemba, na Tuchel anaamini ratiba imekuwa ngumu kwao hasa kutokana na kukabiliwa na majeruhi.

"Ratiba tuliyonayo ni ngumu," alisema. "Wakati huo huo tunakabiliwa na majeruhi, kwanza kwenye kiungo na pili kwenye safu ya ushambuliaji na walinzi.

"Tumekuwa kwenye wakati mgumu kukabiliana na hali hiyo na ndio maana tumeshindwa kuwa na matokeo mazuri."

Baada ya kipigo cha 1-0 kutoka kwa Manchester City wikiendi iliyopita na sare ya 1-1 dhidi ya Brighton Jumanne, kocha huyo wa zamani wa Borussia Dortmund aliwapa siku mbili za mapumziko wachezaji wake ili kujiandaa na mchezo dhidi ya Spurs.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
TOTTENHAM
1 | 1.68
X | 3.85
2 | 4.90

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CONTE AITAKA SPURS KUTUMIA USHAURI WA KANE



**LONDON, England**

ANTONIO Conte ameshauri mabosi wa Tottenham kusikiliza kuhusu ushauri wa usajili kama alivyoshauri Harry Kane kwamba, "klabu inatakiwa kufanya usajili.

Tangu Conte kutua Spurs Novemba, timu hiyo haijaruhusu bao kwenye mechi tano za Ligi Kuu.

Uboreshaji umekuwa mkubwa ikilinganishwa na mwanzo mbaya wa msimu chini ya Nuno Espirito Santo, na dirisha la uhamisho ni wakati Conte anaweza kufanya marekebisho zaidi kwenye kikosi alichorithi.

Tanguy Ndombele anaweza kuwa njiani kuelekea Paris Saint-Germain kwa mkopo, na Conte amegundua kipaji anachotaka kuleta kwenye uwanja wa Tottenham Hotspur.

"Kusema kweli, ninapendelea kuzungumza juu ya mada hii kila wakati na klabu," Conte alisema Ijumaa.


"Kwa hakika, nilifanya tathmini kuhusu kikosi, lakini nimezungumza na klabu na natumaini itanisikiliza."

Bosi huyo wa zamani wa Inter alifanikiwa kutwaa taji la Serie A baada ya kuungwa mkono kwenye soko la usajili, na kuweza kuwasajili wachezaji kama Romelu Lukaku, Achraf Hakimi na Christian Eriksen.

"Nadhani ni muhimu kwa kila klabu kushinda mataji, na wakati huo huo unapaswa kuelewa ikiwa uko tayari kushinda," alisema Conte.

"Kila klabu inaweza kusema, 'Ndio, nataka kushinda mataji', lakini unapaswa kuelewa vizuri ni nini uhakika wako, uko wapi na kisha njia ambayo unapaswa kufuata ili kujaribu kuwa na ushindani na kushinda."

# Fati aipa pigo Barcelona



**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona itamkosa Ansu Fati kwa kipindi kirefu cha baada ya kukumbwa na majeraha.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania mwenye umri wa miaka 19 amekuwa na bahati mbaya kutokana na majeraha na alionekana kutokwa na machozi alipotolewa kwenye mechi ya Copa del Rey dhidi ya Athletic Bilbao, Alhamisi.

Fati alikuwa ametoka kwenye benchi baada ya saa moja tu lakini ikabidi abadilishwe mapema katika muda wa ziada, huku Barcelona wakisema baada ya mchezo huo alipata "jeraha la sehemu ya paja lake la kushoto".

Barcelona walisema katika taarifa yao: "Uchunguzi uliofanywa kwa Ansu Fati Ijumaa ulithibitisha kwamba ana jeraha la karibu la msuli wa paja la mguu wake wa kushoto."

Gazeti la Mundo Deportivo liliripoti kuwa klabu hiyo imependekeza Fati afanyiwe upasuaji.

Kijana huyo ameshiriki katika michezo 10 pekee katika mashindano yote msimu huu, na alikuwa amerejea hivi majuzi kutoka kwa jeraha la misuli ya paja lililodumu kwa miezi miwili.

Hapo awali Fati alikaa nje ya uwanja kwa miezi 10 kutokana na jeraha baya la goti, akirejea Barcelona Septemba msimu huu.

Licha ya uchezaji wake mdogo, Fati ndiye mfungaji bora wa pili wa Barcelona kwa msimu 2021-22 akiwa na mabao matano.

## HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# TANZANITE KUIVAA ETHIOPIA

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 20, (Tanzanite), kinashuka dimbani leo dhidi ya Ethiopia, ukiwa ni mchezo wa raundi ya nne kufuzu kombe la dunia chini ya Costa Rica.

Mchezo huo utakaopigwa uwanja wa Amaan Visiwani Zanzibar na marudiano utachezwa kati ya Februari 4-6, 2021.

Kocha wa kikosi hicho, Bakari Shime amesema wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo kuhakikisha wanapata matokeo mazuri kama ilivyo kwa michezo iliyopita.

Alisema Zanzibar ni sehemu ya Tanzania hivyo wanacheza katika uwanja wa nyumbani na malengo yao makubwa ni kupata ushindi mzuri ili mechi ya marudiano iwe rahisi.

"Kwa muda wa wiki moja tuliokuwepo hapa Zanzibar tumefanya maandalizi ya kutosha, mchezo utakuwa mgumu na ushindani mkubwa kwa sababu Ethiopia sio timu ya kuibeza," alisema Shime.

Alisema wameona ubora wa wapinzani wao na kuhakikisha wanapambana katika mchezo huo kutafuta matokeo chanya ili kuwa rahisi katika mchezo wa marudiano.

Shime alisema kazi kubwa ambayo ameikamilisha kuelekea mchezo huo ni safu yake ya ushambuliaji kwa kuwa makini kutumia nafasi wanazotengezea kupata mabao.

"Tukipata nafasi na kuzitumia vizuri na kupata ushindi mkubwa inakuwa rahisi katika mchezo wetu wa marudiano ambao tutacheza ugenini, kwa sababu Ethiopia iko vizuri na tunawaheshimu," alisema.

Tanzanite inashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kuiondoa Burundi kwenye raundi ya tatu kwa ushindi wa jumla ya michezo miwili kwa mabao 4-3.

Katika mchezo wa mkondo wa kwanza uliochezwa Dar es Salaam, iliibuka na ushindi wa mabao 3-2 na marudiano uliochezwa Desemba 18, mwaka jana, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.



Vijana wanaolelewa katika Kituo cha michezo cha Jakaya Kikwete Jijini Dar es Salaam wakifanya mazoezi kwenye viwanja hivyo jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ushindi aahidi mazuri Yanga

**Na Saada Akida**

WAKATI kikosi cha Yanga kinashuka dimbani leo kusaka pointi tatu dhidi ya Polisi Tanzania, Winga wa Wanajangwani hao, Chiko Ushindi amesema ujio wake ni kuongeza nguvu na makali ndani ya timu hiyo kufikia malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ushindi alisema, akili yake imeshajiandaa kuitumikia Yanga na anajua kila kitu anachotakiwa kufanya ili kuongeza nguvu na kushirikiana na wenzake katika kikosi cha vinara hao wa Ligi.

Alisema ana imani kubwa na uwezo wake na atahakikisha anafanya kile ambacho wengi wanatarajia kutoka kwake.

"Nimezungumza na Kocha wa Yanga, Nesreddine Nabi na amenitaka nije kuongeza kasi ya upatikanaji wa mabao nikitokea pembeni, sina wasiwasi na uwezo wangu," alisema Ushindi.

Alisema ana imani na uwezo wake kuhakikisha anatengeneza nafasi kwa wenzake na endapo atapata nafasi atahakikisha anapambana kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 23/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 5839 | NEC Nijmegen vs Feyenoord | 7.47 | 4.91 | 1.35 |
| 14:30 | 3137 | Cagliari vs Fiorentina | 5.01 | 4.10 | 1.62 |
| 15:00 | 3115 | Metz vs Nice | 4.49 | 3.84 | 1.72 |
| 15:30 | 3291 | Hannover vs Dynamo Dresden | 2.15 | 3.19 | 3.33 |
| 16:00 | 1226 | Granada vs Osasuna | 2.51 | 3.16 | 2.91 |
| 16:00 | 5240 | Burgos vs Leganes | 2.75 | 3.09 | 2.55 |
| 16:30 | 1467 | PSV Eindhoven vs Ajax | 3.50 | 3.59 | 1.94 |
| 17:00 | 1023 | Spezia vs Sampdoria | 2.69 | 3.29 | 2.60 |
| 17:00 | 1638 | Clermont Foot vs Rennes | 3.98 | 3.69 | 1.84 |
| 17:00 | 1740 | Bordeaux vs Strasbourg | 3.68 | 3.73 | 1.90 |
| 17:00 | 2155 | Angers vs Troyes | 2.07 | 3.18 | 3.73 |
| 17:00 | 2440 | Napoli vs Salernitana | 1.15 | 7.80 | 16.00 |
| 17:00 | 2729 | Leicester vs Brighton | 2.55 | 3.30 | 2.75 |
| 17:00 | 3207 | Crystal Palace vs Liverpool | 5.22 | 4.21 | 1.58 |
| 17:00 | 3355 | Arsenal vs Burnley | 1.41 | 4.53 | 7.77 |
| 17:00 | 4782 | Nantes vs Lorient | 2.12 | 3.14 | 3.64 |
| 17:00 | 5267 | Torino vs Sassuolo | 2.11 | 3.55 | 3.30 |
| 17:00 | 5838 | Apoel Nicosia vs Aris Limassol | 1.85 | 3.46 | 4.16 |
| 17:30 | 5696 | RB Leipzig vs VfL Wolfsburg | 1.51 | 4.39 | 5.78 |
| 18:00 | 2556 | Linense vs Gimnastic Tarragona | 2.24 | 3.04 | 3.09 |
| 18:00 | 5783 | Sporting Gijon vs Amorebieta | 1.84 | 3.28 | 4.31 |
| 18:15 | 2112 | Atromitos vs AEK Athens | 5.32 | 3.54 | 1.65 |
| 18:15 | 3923 | Real Madrid vs Elche | 1.21 | 6.34 | 13.20 |
| 18:15 | 5064 | Volos vs PAOK | 4.24 | 3.55 | 1.79 |
| 18:15 | 5801 | Vicenza vs Cittadella | 2.98 | 3.18 | 2.33 |
| 18:30 | 5476 | Maritimo vs Belenenses | 1.80 | 3.41 | 4.44 |
| 18:30 | 5709 | Rio Ave vs Sporting Farense | 1.83 | 3.33 | 4.21 |
| 18:30 | 5881 | Vitoria Guimaraes vs GD Estoril | 1.92 | 3.40 | 3.84 |
| 18:45 | 5640 | Sparta Rotterdam vs Utrecht | 3.43 | 3.33 | 2.05 |
| 19:00 | 1864 | Galatasaray vs Trabzonspor | 2.51 | 3.20 | 2.75 |
| 19:00 | 3967 | Burkina Faso vs Gabon | 2.77 | 2.82 | 2.82 |
| 19:00 | 5794 | Badalona vs CD Ebro | 2.12 | 2.75 | 3.76 |
| 19:05 | 4852 | Montpellier vs Monaco | 3.49 | 3.44 | 2.05 |
| 19:30 | 4543 | Chelsea vs Tottenham | 1.68 | 3.85 | 4.90 |
| 19:30 | 5161 | Hertha BSC vs Bayern Munchen | 9.93 | 6.56 | 1.23 |
| 20:00 | 5467 | Empoli vs Roma | 3.85 | 4.10 | 1.80 |
| 20:15 | 3959 | Huesca vs Ponferradina | 2.25 | 3.05 | 3.25 |
| 20:15 | 4918 | Girona vs Lugo | 1.70 | 3.45 | 4.92 |
| 20:30 | 1611 | Olympiakos vs PAS Giannina | 1.31 | 4.73 | 9.86 |
| 20:30 | 1932 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.75 | 2.95 | 2.80 |
| 20:30 | 3402 | Lecce vs Cremonese | 2.05 | 3.19 | 3.58 |
| 20:30 | 3693 | Mechelen vs Anderlecht | 4.05 | 3.85 | 1.76 |
| 20:30 | 4851 | Real Sociedad vs Getafe | 1.65 | 3.55 | 5.80 |
| 21:00 | 1516 | Gil Vicente vs Portimonense | 2.03 | 3.25 | 3.64 |
| 22:00 | 3559 | Nigeria vs Tunisia | 1.89 | 3.08 | 4.66 |
| 22:45 | 2176 | Paris St Germain vs Reims | 1.25 | 5.72 | 10.73 |
| 22:45 | 5098 | AC Milan vs Juventus | 2.64 | 3.29 | 2.64 |
| 23:00 | 1063 | Alaves vs Barcelona | 5.12 | 3.97 | 1.63 |
| 23:00 | 5952 | Alcorcon vs Mirandes | 2.65 | 3.09 | 2.65 |
| 23:30 | 4838 | Porto vs Famalicao | 1.20 | 6.35 | 11.90 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Januari 23, 2022
Nipashe



## Tuchel: Chelsea itasajili Januari hii

HABARI UK 21




Mlinzi wa Simba, Shomary Kapombe akiwania mpira dhidi ya Salum Kihimbwa wa Mtibwa Sugar wakati wa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baina ya timu hizo uliopigwa jana uwanja wa Manungu, Morogoro. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YAVUTWA

●●● Yalazimishwa sare na Mtibwa uwanja wa Manungu huku...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi Simba, jana wameshindwa kuchukua pointi tatu kwa mara nyingine tena, baada ya kulazimishwa suluhu na Mtibwa Sugar, mechi ikichezwa kwa mara ya kwanza baada ya miaka 23, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, Morogoro.

Wakati wanachama na mashabiki wa timu hiyo wakitegemea kujiliwaza kwa pointi tatu baada ya kupoteza mechi Jumatatu iliyopita dhidi ya Mbeya City kwa bao 1-0, walijikuta hawaamini macho na masikio yao, baada ya kipenga cha mwisho kupulizwa, ikishindwa kufunga bao kwenye mechi mbili mfululizo.

Ni mechi iliyochezwa kwenye kiwanja chenye nyasi nzuri, lakini kilichokuwa na maji yaliyotuama na matope kutokana na mvua kubwa kunyesha kabla ya mechi hiyo.

Kiungo mshambuliaji wa Simba, Clatous Chama alicheza kwa mara ya kwanza tangu aondoke nchini kwenda kujiunga na RS Barkane ya Morocco, na kurudishwa kwenye kipindi cha dirisha dogo la usajili. Aliingia mwanzoni mwa kipindi cha pili na kucheza kwa dakika 45 zilizobaki.

Mechi ilianza kwa Mtibwa Sugar kuchangamka zaidi kuliko Simba na iliwachukua dakika 30 kuweza kufanya shambulizi la kwanza langoni mwa wenyeji wao.

Straika aliyerejea tena Mtibwa Sugar kwenye kipindi cha dirisha dogo, Hamad Hilika, aliambaa na mpira kwenye winga ya kulia dakika ya tano baada ya mchezo kuanza na kupiga krosi ambayo ilitemwa na Kipa Aishi Manula, lakini hakukuwa na mtu yoyote karibu, akaurudia tena kuudaka.

Dakika nne baadaye kiungo anayecheza kwa mkopo akitokea timu hiyo ya Simba, nusura awaadhibu waajiri wake wakuu, baada ya kuupata mpira akiwa karibu na lango, lakini kabla hajapiga shuti, Manula alitokea kwenye kuokoa, wakagongana na wote kuuacha mpira ukiambaa bila mwenyewe, kabla ya Joash Onyango kuutokea na kuufagia kwenye hatari.

Bado, Mtibwa Sugar iliendelea kulitia msukosuko lango la Simba, kwani dakika ya 16, pasi mbovu ya Mzamiri Yassin, ilimkuta Hassan Kihimbwa ambaye alimmegea Kelvin Sabato na kuleta kizaazaa golini kabla ya kuokolewa.

Hatimaye Simba ilifanya shambulizi la kwanza langoni mwa Mtibwa Sugar dakika ya 30, ambalo nusura Hassan Banda ajifunge mwenyewe, alipopiga kichwa kuokoa krosi ya Sadio Kanoute, lakini golikipa Shaaban Kado aliruka juu na kuupiga ngumi mpira uliokuwa unaelekea wavuni, ukatoka kona.

Hassan Dilunga alishindwa kuipatia Simba bao dakika ya 39, alipobaki yeye na Kado, akapiga shuti dhaifu ambalo lilidakwa bila shida na kipa huyo.

Dakika moja kabla mapumziko, Dilunga tena alipiga shuti kali, akiwa umbali kiasi cha mita 25, lakini mpira ukatoka juu kidogo ya lango, ukiwa umeshampita Kado.

Kipindi cha pili licha ya kila timu kufanya mabadiliko, ambayo kwa kiasi fulani yaliisaidia Simba kufanya mashambulizi ya mechi, lakini hayakuisaidia kupata bao.

Ni kipindi ambacho Simba ilikosa mabao matatu ya wazi, dakika mbili baada ya mapumziko, Kagere alipiga shuti lililopanguliwa na Kado alifanya kazi ya ziada kuzuia shuti la Pape Sakho na dakika za nyongeza, Shomari Kapombe alikaribia kuiandikia timu yake bao, lakini shuti lake lilitoka pembeni kidogo mwa lango.

Ni matokeo yanayoifanya Simba kuendelea kukaa nafasi ya pili, lakini sasa ikiwa na pointi 25, ikiwa imezidiwa pointi saba na vinara wa Ligi Kuu Yanga yenye pointi 32, kabla ya mechi yake ya leo dhidi ya Polisi Tanzania.

Mtibwa Sugar inakamata nafasi ya 13, ikiwa na pointi 12 kwa mechi 13 ilizocheza.

## Yanga mikononi mwa Polisi Tanzania leo

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga, leo watakuwa wageni kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha kucheza dhidi ya Polisi Tanzania kwenye mechi ya raundi ya 13 ya ligi hiyo.

Awali mechi hiyo ilikuwa ichezwe kwenye Uwanja wa Ushirika mjini Moshi mkoani Kilimanjaro, lakini imeripotiwa kuwa unatumika kwa matumizi mengine.

Yanga itakuwa inajaribu kushinda mechi ya tano mfululizo, ikiwa imefanya hivyo mara nne dhidi ya Prisons na Biashara United ikishinda mabao 2-1, ikiichapa Dodoma Jiji mabao 4-0 na mara ya mwisho ikiichabanga Coastal mabao 2-0 Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Mkwakwani Tanga.

Vinara hao wamekuwa wakishinda mfululizo tangu walipotoka suluhu bila kufungana dhidi ya watani zao wa jadi Simba Desemba 11 mwaka jana.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi amesema kuwa mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu Polisi Tanzania ni timu nzuri, inafanya vema kwenye ligi na ndiyo maana baada ya mechi dhidi ya Coastal Union hakutaka timu irejee Dar es Salaam, badala yake iende Arusha kwa ajili ya maandalizi.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze naye hakutofautiana sana na mkuu wake.

"Utakuwa mchezo mgumu, Polisi Tanzania iko kwenye nafasi ya nne na imeanza ligi vizuri, na ina mastraika wazuri, ila sisi tumejiandaa kwenye mechi ngumu, mipira mirefu na viwanja ambavyo si rafiki. Tunaamini kuwa tutakuwa na mechi nzuri na tutachukua pointi tatu," alisema raia wa Burundi.

Naye Kocha msaidizi wa Polisi Tanzania, George Mketo amesema wao wamejiandaa kucheza kwenye uwanja wowote ule na kwamba wana wachezaji wazoefu wa kuweza kuikabili Yanga bila matatizo.

"Mpira wa Kitanzania tunacheza kwenye kiwanja chochote, ni namna ambavyo timu imejiandaa tu kwenye mechi husika. Tumeshawahi kucheza kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid si mara moja wala mbili. Tunakwenda kucheza na timu inayoongoza ligi, tunaiheshimu, ina walimu wazuri na wachezaji bora, lakini na sisi wachezaji wetu ni wazoefu sana kwenye ligi, wameshacheza kwenye klabu mbalimbali kubwa za Ligi Kuu kwa hiyo na sisi tumejiandaa na tunakwenda kukabiliana nao," alisema kiungo huyo wa zamani wa Simba.

Polisi Tanzania itaingia dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa suluhu Jumatatu iliyopita dhidi Namungo.

Timu zote mbili zinaingia uwanjani zikiwa zimecheza mechi 12, Yanga ikiwa kileleni kwa pointi 32, huku Polisi Tanzania ikiwa kwenye nafasi ya nne kwa pointi 18, ikishinda mechi nne, sare sita na imepoteza mechi mbili.

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042